


# EP EBOOKS

This document is tracked, do not share

# MALENGA WA KENYA

**Kwa shule za Msingi**

**(Mtalaa mpya wa umilisi)**

**Wahariri**

**Timothy Omusikoyo Sumba**
**Dkt. Jackline Murimi**
**Kaka Fred**

HAKIMILIKI ©2021 **NA Timothy Omusikoyo Sumba**

Haki zote zimehifadhiwa. Nimarufuku na hatia kwa wenye silica za kugushi, kuiga, kubadili, kuchapisha, kutafsiri, kuigiza au kutumia mbinu zozote bila idhini ya mwandishi kupitia kwa wakili kulingana na (*Copyright, Design and Patents Act)* ya 1988.

Mtu yeyote atakayefanya kitendo chochote kinyume na sheria anaweza kushtakiwa.

Toleo la kwanza: Machi 2021

Kimechapishwa na Elong'o Publishers

P.O BOX 944, Narok

Baruapepe: info@elongopublishers.co.ke

Rununu: +254742433826

**ISBN: 9798728310587**

# UTANGULIZI

Malenga wa Kenya ni diwani ya ushairi kwa hadhira lengwa ya shule za msingi hususan wanafunzi wa gredi za nne hadi sita. Tungo za kisasa zinazoukumbatia mtaala mpya wa elimu - umilisi zimetawala. Mada kuu zimedondolewa silabasini ili kutungiwa mashairi mwafaka. Isitoshe, msamiati tangulizi ni ule sahili uliooneshwa silabasini ili mwanafunzi aanzie kwa ajuayo kabla ya kukabiliana na wastani kisha mengineyo ya kumfikirisha zaidi. Mashairi mengi yaliyosheheni ubunifu yanasisimua hadi ya kusisimua. Kimsingi, azma ya washairi ni kuelimusha kwa ucheshi, burudani na kimchezo. Utafiti waonyesha kuwa kusoma kwa aina hii hakuchoshi akili.

Ushairi ni nguzo kuu katika fasihi ya watoto wenye kiu ya kujua na Kufahamu mzo wa mambo. Matumaini yetu ni kuwa kwa kusomasoma, na kughanighani mashairi aina ya tathnia, tathlitha, tarbia, takhmisa, tasdisa ngonjera na guni wanafunzi watajichotea ubunifu utakaowafanya Malenga, manju na waghani wa kupigiwa mifano.

Timothy Omusikoyo Sumba,
*Mwandishi, mwalimu mshauri na mhariri wa kazi bunilizi.*

# MALENGA WA KENYA

**1. Viungo vya Mwili....Dkt. Jackline Murimi (*Malenga Mbunifu),* NAIROBI**

**2. Heshima sio utumwa..Elisha Otoyi (*Malenga wa Wanyonge*), HOMABAY**

**3. Mazingira.....................Georgina Nyatichi (*Bi. Makini*), NYAMIRA**

**4. Elimu...........................Alfred Lobawoi ( *Mweledi Chipukizi*), TURKANA**

**5. Majina ya misimu......Christopher Kalunda (*Malenga Mwepesi*), VIHIGA**

**6. Naionea fahari............Ali M. Mwanza (*Malenga Kande*) KWALE**

**7. Haki za watoto...........Lilian Alividza (*Malkia wa Nyikani*), KAKAMEGA**

**8. Ukulima ndiyo kazi.....Kaka Fred (*Malenga wa Dhahabu*), BUNGOMA**

**9. Mzalendo mimi..........Vincent Imbali (*Malenga Mwona Mbali*), VIHIGA**

**10. Si hoja yetu jinsia?...Sophie Binsari (*Tarabizuna ya Jangwani*), KISII**

**11. Makao......................Okwalo Wambani (*Malenga wa mitume*), BUSIA**

**12. Tupinge ugaidi........Agadias Ikoha (*Malenga wa Nyali one),* MOMBASA**

**13. Mshikamano wa taifa...Henry Momanyi (*Ustadh Momanyi*), TRANSNZOIA**

**14. Lishe bora...............Michael Cosmas (M*alenga wa sayari kavu*), KITUI.**

**15. Nakupenda Ushairi...Timothy Sumba (*Malenga* mtaarabu), KAKAMEGA**
**16. Tujifunze Tashbihi.....Bright Odeng (*Nuru Gizani*), SIAYA**
**17. Hisabati.................Willyberforce Keya (*Malenga wa Musanda*), KAKAMEGA**
**18. Methali za Kiswahili....Derrik Masika (*Dokta Ziro*), KAKAMEGA**
**19. Adabu akiba................Wafula P Wanjala (*Mvua ya Njaa*), KAKAMEGA**
**20. Tulinde mazingira...... Erick Omondi (*Babu Mesh*), SIAYA**
**21. Hatutaki Siasa Mbi.............Philip Opetuh *(malenga mstahiki*), NAIROBI**
**22. Lindeni Vyoo..................Alex Simiyu ( *Ustadh Kiamboni),* TRANS-NZOIA**
**23.Jipe moyo...............Kelvin Njoroge ( *ustadh Muturi)* TRANS-NZOIA**
**24. Ndimi mtambi natamba.....John Ngari (*Malenga mji mkuu),* EMBU**
**25. Mama yangu .............. Stephen Oluoch ( *Anzalisteve*), MIGORI**

**VIUNGO VYA MWILI**

**Mtunzi: Dkt. Jackline Murimi**
**Lakabu: Malenga Mbunifu**
**Mhadhiri wa Kiswahili Chuo Kikuu cha Tom Mboya.**

Moyo wangu warindima, mapigo utaratibu,
Mishipa damu wapima, mipango kuiratibu,
Barabara mtima, vena ateri zajibu,
Shukrani zangu kalima, uhai tele kunipa.

Mapafu tena mawili, kushoto na kuliani,
Oksijeni tia mwili, hewa safi vuta ndani,
Yasafiri kwenye seli, damu nyekundu mwilini,
Shukrani zangu Jalali, uhai tele kunipa.

Ini kiungo mwilini, kikuu kati ya vingine,
Kushotoni kuliani, sehemu megawikane,
Sumu ondoa mwilini, kati ya kazi zingine,
Shukrani zangu Molani, uhai tele kunipa.

Figo ni viungo jozi, umbole ja haragweni,
Kaziyo figo iwazi, mkojo unda mwilini,
Chunga damu shinikizi, chumvi na maji pimani,
Sukrani zangu mwokozi, uhai tele kunipa.

Ubongo ndo kazi yako, viungo kuelekeza,

Umo katika kichwako, misuli kuiongoza,
Kudhibiti mwendo wako, ujumbe kuuwaza,
Shukrani zangu Rabuko, uhai tele kunipa

Kaditamati natua, japo vimesalia viungo,
Inshalla tafafanua, ipo siku kwa mtungo,
Muhimu kutambua, kutunza kila kiungo,
Shukrani zangu wazijua, uhai tele umenipa.

**USAFI**
**Mtunzi: Elisha Otoyi (*Isah Bin Omar*)**
**Lakabu: Malenga wa Wanyonge**
**Gatuzi : Homabay**

Msichana mvulana, nimejawa na uhondo,
Maswali magumu sina, katika wangu muundo,
Iwapo tutapatana, taboresha zetu nyendo,
Kati yako na usafi, nani hujali mwenziwe?

Chunguza yako mavazi, ambayo unayavaa,
Niambie waziwazi, iwapo yanakufaa,
Wayafua kwa ujuzi, hata yakose balaa,
Kati yako na usafi, nani hujali mwenziwe?

Bombo dogo walijua, ninasema ile kocho,
Je,walishughulikia, yatazame yangu macho,
Mara ngapi walifua, usiyaende naficho,
Kati yako na usafi, nani hujali mwenziwe?

Waonaje patipati, za shule au nyumbani,
Zinatisha ja mauti, kwa uvundo ulo ndani?
Zikoje kila wakati, soli zenu nijubuni,
Kati yako na usafi, nani hujali mwenziwe?

Sikuacha mwanadada, nisije kuitwa chizi,
Ndoo ufanye shuhuda, kuhusu hiyo shumizi,

Wajua zake faida, hebu kwako nimaizi,
Kati yako na usafi, nani hujali mwenziwe?

Mengineyo kama tai, shati hadi suruali,
Hili deni nakudai, naomba ulikubali,
Kuziosha hukosei, maisha yako najali,
Kati yako na usafi, nani hujali mwenziwe?

Tamati ya kaditama, ukingoni nimetuwa,
Kuwaambia ni vyema, na muishi mkijuwa,
Epusheni hiki chama, usafi kuzingatiwa,
Kati yako na usafi, nani hujali mwenziwe?

**JITATHMINI**

1. Shairi hili lina beti ngapi?
2. Taja vitamkwa sawa vya ubeti wa tatu
3. Atungaye shairi ana majina mawili. Yataje
4. Hili ni aina gani ya shairi? Eleza
5. Ubeti wa pili kwa jumla una mizani mingapi?

**HESHIMA SIYO UTUMWA**
**Mtunzi: Elisha Otoyi (Isah Bin Omar)**
**Lakabu: Malenga wa Wanyonge**
**Gatuzi : Homabay**

Hujambo wangu msena, salamu iwe awali,
Ninayo tele kunena, naomba chako kibali,
Tuweze kusemezana, kuyahusu maadili,
Malimwengu niloona, nachelea kuyakuli,
Utu ule wa zamani, kawendapi nauliza.

Mamkizi ya adabu, yaliyokuwa zamani,
Nyakati hizo za babu, kwa mfano buriani,
Aliniambia abu, litumika salamuni,
Kuionesha adabu, mkikutana njiani,
Mkiwa munaagana, muda 'refu tapezana.

Salam aleikhumu, ilidumisha amani,
Na kuleta hata hamu, kuchangia ukumbini,
Salama na ikadumu, kwake mja maishani,
Si ile ya binadamu, nasema ya Maanani,
Jibu lake nalienzi, aleikhum salam.

Ndugu yangu waambaje, vile vile litumika,
Maanake wasemaje, kauli zako ataka,
Nakuuliza iweje, umjibu kama taka?
Yuajibu wadaije, yakini nahuzunika,

Hili ndilo jibu lake, sina jambo la kuamba.

Jingine mchana mwema, wakati wa adhuhuri,
Mambo na yawe salama, taraa yanapojiri,
Pengine unaposoma, sipate mbaya habari,
Neno hili kilipima, nalo powa gani zuri?
Usihofu mbasi wangu, taitika inshalla.

Tujipigeni misasa, umendapi utu wetu,
Ni wapi tulipokosa, ama tuwende msitu?
Mbona mnajimamasa, toweni hili boriti,
Tusiweze kujinasa, tungali tuna wakati,
Mithali yetu ya leo, heshima siyo utumwa.

**JITATHMINI**

1. Shairi hili ni la aina gani? Eleza
2. Mshororo wa mwisho katika kila ubeti wa shairi hili huitwaje?
3. Nini maana ya malimwengu lilivyotumika katika shairi?
4. Dondoa maamkuzi yaliyo katika shairi na majibu yao
5. Kwa nini malenga alitunga shairi hili?

**NYUMBA YETU**
**Mtunzi: Elisha Otoyi (Isah Bin Omar)**
**Lakabu: Malenga wa Wanyonge**
**Gatuzi : Homabay**

Nyumba yetu hupendeza, vyumba sita vimo humu,
Sebule nikiiwaza, sisahau na hamamu,
Jikoni mnapendeza, mmejawa majukumu,
Sitaweza kuvisaza, dari na hata fremu.

Wazazi wamenunua, vitu tele humo ndani,
Globu  twazitumia, kuangaza makaoni,
Tumbuu inatufaa, kwa usalama langoni,
Kizingiti tukingia, wahalifu wa gizani.

Pa kulala ni pazuri, vitanda ni vya Kizungu,
Neti zetu kwenye dari, twatandaza wangu wangu,
Matendegu ni mazuri, ukitazama mvungu,
Hewa safi furifuri, mejaza kitanda changu.

Wageni wanapokuja, sebule hukaribisha,
Wajadili zao hoja, mambo yao ya maisha,
Humo kwao ni faraja, furaha pia bashasha,
Mama yetu bi. Hadija, kila mara asafisha.

Jikoni kunazo kuni, kinu mchi na makaa,
Mafiga ya kizamani, humo ndani yatufaa,

Nashukuru Maanani, kuweza kutuokoa,
Nyumba yetu kwa yakini, imeweza tukomboa.

Piga deki nitazidi, usafi utatawala,
Hata kama ni baridi, hili jambo ni aula,
Kukupenda sina budi, nakupenda ja chakula,
Naomba rusa kurudi, kusafisha pa kulala.

**JITATHMINI**

1. Vifungu vya shairi huitwaje?
2. Kwa nini Malenga ametumia *Maanani* badala ya *Manani*?
3. Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika shairi
   Tumbuu, Wangu wangu
4. Shairi hili huitwaje?
5. Taja utao wa mloto wa ubeti wa nne

**BARUA YANGU**
**Mtunzi: Elisha Otoyi (Isah Bin Omar)**
**Lakabu: Malenga wa Wanyonge**
**Gatuzi : Homabay**

Pokea salamu zangu, uko hali gani mama?
Ninamshukuru Mungu, kwani kanilinda vyema,
Ninayo maneno chungu, kukupasha nilosoma.

Barua ya kirafiki, mwalimu metufundisha,
Poteza muda sitaki, kwa kuwa umeshaisha,
Makinika hino wiki, sitoweza kukuchosha.

Nataka kuelezea, jinsi tunaiandika,
Anwani waianzia, moja tu inotajika,
Juu juu ya kulia, ni hapo unaiweka.

Tarehe siyo sehemu, au moja ya anwani,
Jina la shule muhimu, na tokako duniani,
Ilobaki ni rakamu, zake posta gatuzini.

Kushoto ninakuwenda, jina lake nitataja,
Ambaye ninampenda, sentensiye inakuja,
Kwa mfano nana Brenda, au Daktari Elija.

Maamkuzi nacheza, kwa njia yenye adabu,
Mistari naendeleza, huku nikiihesabu,

Aya moja nikijaza, imemtosha muhibu.

Aya zile zifatazo, zinakuwa za malengo,
Nayataja kwa mkazo, bila kusema uwongo,
Ya mwisho ndiyo himizo, nikiufika ukingo,

Namalizia kwaheri, msenangu kimuaga,
Asipatane na shari, nimtolee uoga,
Atawaliwe na kheri, ishi marefu ja twiga.

'husiano nitatiya, nikifika tamatini,
Jina langu laingiya, laja mwisho hapo chini,
Kaditama mefikiya, familia kwayerini.

**JITATHMINI**

1.Taja kichwa cha shairi hili
2. Mloto wa ubeti wa tano ni upi?
3. Shairi hili halina kibwagizo. Jadili
4. Kulingana na malenga, angazia vipengele vya anwani.
5. Eleza vile mbinu ya inkisari ilivyotumika.

**JINA LANGU SEMA WEWE**
**Mtunzi: Elisha Otoyi (Isah Bin Omar)**
**Lakabu: Malenga wa Wanyonge**
**Gatuzi : Homabay**

Hata kama hunitaki, nitakugusa moyoni,
Ninajua utabaki, nyuma mwako maishani,
Nipo kukupiga jeki, ufaulu aushini,
Nitakupa yako haki, jina langu nalo nani?

Ukienda Nairobi, ninatumika garini,
Tembelea Magharibi, na upande wa Kusini,
Je wawajua manabi, tabiri nawaauni,
Niliumbwa naye Rabi, alipokuwa mbinguni.

Elekea Mashariki, tanitumia rubani,
Na Kusini Mashariki, chini chini taifani,
Potea kwenye tariki, ufanye hivyo kwa nini?
Nakupenda we rafiki, jina langu nambieni.

Umbo langu ndilo hili, mistari mbili gaweni,
Kunichora siyo ghali, unganisha hizo wani,
Kinisoma kwa umbali, nina mishale nchani,
Ni rahisi hili swali, mkitilia manani.

Majira ninatumika, rafiki  kuwatajeni,
Upande unaotoka, bila mimi huwezani,

Waweza kunikumbuka, Mashariki mwa Kusini?
Wanifanya kukucheka, ati hujui mi nani.

Kwaheri ninakuaga, nimefika ukingoni,
Nikaende kwenye uga, Magharibi ya Kusini,
Kisha naenda kuoga, Mashariki ya Kusini,
Nyumbani ukila mboga, jina langu mtajeni.

**JITATHMINI**

1. Taja jina la mhusika wa shairi hili
2. Andika kituo cha ubeti wa tatu
3. Ukwapi wa mleo wa ubeti wa tano ni upi?
4. Mhusika wa shairi hili ana faidi chungu kwa wanadamu. Zitaje
5. Mbona malenga ametumia manabi badala ya manabii?

**MAZINGIRA**
**Mtunzi: Georgina Nyatichi**
**Lakabu: Bi. Makini**
**Gatuzi : Nyamira**

Mazingira hazina yetu, sisi sote binadamu,
Tuyatunze kule kwetu, na hata shuleni muhimu,
Tusihofu wote katu, kuyahifadhi yadumu,
Tuyatunze mazingira, jamani jambo muhimu.

Mkiwa bado shuleni, wajibikeni vilivyo,
Haja zako zitimizeni, kubwa ndogo ipasavyo,
Maji yakiwa chooni, takasa takikanavyo,
Tuyatunze mazingira, jameni jambo muhimu.

Nawa maji na sabuni, unapotoka chooni,
Kunawa sikimbieni, maagizo fuateni,
Chooni mna viini, vinadhuru afya ndani,
Tuyatunze mazingira, jameni jambo muhimu.

Wanafunzi darasani, ovyo situpe taka,
Chonga penseli mwendani, tumia jaa la taka,
Ukusanye kwa makini, utupwe shimo la taka,
Tuyatunze mazingira, jameni jambo muhimu.

Tunapocheza uwanjani, kumbuka miti yetu,
Matawi sikate chini, taharibu kivuli chetu,

Hewa safi vuta ndani, miti mesafisha kutu,
Tuyatunze mazingira, jameni jambo muhimu.

Napoila ndizi yako, ganda usitupe chini,
Litabwaga tako lako, viungo vyako vunjikani,
Litieni jaa lako, kisha lifike shambani,
Tuyatunze mazingira, jameni jambo muhimu.

Umoja jambo azizi, kuyatunza mazingira,
Wote bila pingamizi, zingatieni imara,
Kwa miaka na miezi, afyani bila kukera,
Tuyatunze mazingira, jameni jambo muhimu.

**JITATHMINI**

1) Shairi hili ni la aina gani? Toa sababu.
2) Taja sehemu za kutupa uchafu kulingana na shairi.
3) Mbona tunawe mkono kwa maji na sabuni tunapotoka msalani?
4) Eleza maneno manne ya kudumisha usafi kulingana na shairi.
5) Kibwagizo cha shairi hili ni kipi.

**ELIMU**
**Mtunzi: Alfred Lobawoi**
**Lakabu: Malenga Mweledi Chipukizi**
**Gatuzi :Turkana**

Elimu naitangaza, ifikie darasani,
Kila kona ninapaza, wa bara hata wa pwani,
Sichelei kuwajuza, yalokuwa ya sirini,
Mizizi yake michungu, matunda yake matamu.

Hakunaye wa kusaza, tajiri kwa masikini,
Pamwe tena kwenye meza, udugu pia amani,
Hakuna cha kutatiza, elimu ni burudani,
Mizizi yake michungu, matunda yake matamu.

Vipaji vinavyokuza, si nesi si marubani,
Wale waliojikaza, wananyota aushini,
Ni wengi wamewekeza, kuibuka medalini,
Mizizi yake michungu, matunda yake matamu.

Haina pa kukatiza, tupaitapo dalini,
Vile vile kuburuza, siyo mwendo wake sini,
Safari yake yajaza, tele akili kichwani,
Mizizi yake michungu, matunda yake matamu.

Huendapo kwenye giza, huzagaa kwa yakini,
Inakupea mwangaza, popote penye tufani,

Huondoa hozahoza, hili ninawapasheni,
Mizizi yake michungu, matunda yake matamu.

Ni funguo yaingiza, popote pale langoni,
Katu halitogeuza, hilo haliwezekani,
Kila nachokiagiza, utayaona ozini,
Mizizi yake michungu, matunda yake matamu.

**JITATHMINI**

1. Hili ni shairi la aina gani?
2. Taja ukwapi wa ubeti wa pili katika mshororo wa kwanza.
3. Eleza vina katika ubeti wa tano.
4. Taja methali moja inayoafiki ubeti wa tano kuhusu elimu.
5. Taja vipaji viwili ambavyo vinakuzwa na elimu.

## MAHALI MBALIMBALI

**Mtunzi: Alfred Lobawoi**
**Lakabu: Malenga Chipukizi Mweledi**
**Gatuzi : Turkana**

Popote pale nchini, sehemu zina majina,
Vijijini na mijini, utaona kwa upana,
Mabango yake someni, mkafahamu kwa kina,
Kule kutembea kwingi, ndiko kuyaona mengi.

Tembea Makavazini, vya kale utaviona,
Vipo vile vya thamani, ambayo hukuyaona,
Wameviweka pembeni, utasoma mengi sana,
Kule kutembea kwingi, ndiko kuyaona mengi.

Vya kula Maabarani, hufanywa kwa uchunguzi,
Watumia hadubini, ikiwa ndiyo mwamuzi,
Huchunguza kwa uzani, nje na ndani ya ngozi,
Kule kutembea kwingi, ndiko kuyaona mengi.

Kule kwa pambajioni, yaweza kuwa nyumbani,
Iwe hata ofisini, aidha sipitalini,
Wateja hukaa chini, kusubiri kwenda ndani,
Kule kutembea kwingi, ndiko kuyaona mengi.

Penye mitambo yaani, nasema Karakanani,
Hutengenezwa samani, kwa maumbo ya kubuni,

Fundi akiwa kazini, hakosi zana jamani,
Kule kutembea kwingi, ndiko kuyaona mengi.

Tunakoita Bafuni, jina lake hamamuni,
Ni pa kukoga mwilini, kwa maji hata sabuni,
Bomba mvua oneni, humwaga maji mwilini,
Kule kutembea kwingi, ndiko kuyaona mengi.

Chumba cha Korokoroni, wapo wale Washukiwa,
Kinyume na Gerezani, Wahalifu tunajuwa,
Tofauti tatueni, msije changanyikiwa,
Kule kutembea kwingi, ndiko kuyaona mengi.

Tama ninatamatisha, mengine utabukua,
Utafiti vya kutosha, zaidi utavijua,
Tembea ninakupasha, mwenzangu utang'amua,
Kule kutembea kwingi, ndiko kuyaona mengi.

**JITATHMINI**

1. Shairi hili ni la bahari gani?
2. Lipe shairi hili kichwa mwafaka.
3. Kulingana na ubeti wa tano, fafanua maana ya pambajio.
4. Taja idadi ya mizani katika ubeti wa kwanza.
5. Ni tofauti gani iliopo baina ya korokoroni na Gerezani kwa mujibu wa shairi hili? Vitaje.

**AFYA!**
**Mtunzi: Alfred Lobawoi**
**Lakabu: Malenga Chipukizi Mweledi**
**Gatuzi : Turkana**

Tunapata kwa chakula, virutubisho tisini,
Kuku kwa maziwa Lala, twaviita Protini,
Matunda tunayokula, twavijua vitamini,
Afya ina manufaa.

Yatutendea jamala, bila ya kuona soni,
Hatusemi ndiyo hila, inatupa afueni,
Tukipata ni hewala, tunakuwa furahani,
Afya ina manufaa.

Yatumika nayo hela, kutafuta madukani,
Iwe rupia na dola, afya nzuri maishani,
Sipitali pia kila, utapata humo ndani,
Afya ina manufaa.

Siha ndiyo yetu sala, tusigonjeke njiani,
Magonjwa tukiwa bila, twamshukuru Manani,
Muhimu hili suala, tutilie maanani,
Afya ina maana.

Kula vitu vya jalala, ni kujitia ta'bani,
Itakupa na madhila, udhoofike ja jani,

Utokapo na msala, ujinawe mikononi,
Afya ina maana.

Pahali pa safi lala, iwe juu ama chini,
Na pasafi iwe ghala, vyombo viwe salamani,
Mwema uwe wa kuola, nasisitiza jueni,
Afya ina maana.

**JITATHMINI**

1. Mshairi anazungumzia yepi kupitia shairi hili?
2. Taja kibwagizo katika ubeti wa tatu.
3. Katika ubeti wa tano ni ujumbe upi mshairi anatupasha?
4. Taja mizani ya kibwagizo la shairi hili.
5. Eleza kisawe cha neno Afya.

**MAGONJWA!**
**Mtunzi: Alfred Lobawoi**
**Lakabu: Malenga Chipukizi Mweledi**
**Gatuzi : Turkana**

Magonjwa natanguliza, wanafunzi fahamuni,
Athari zinotatiza, mwili wetu Insani,
Kinga inavyopunguza, yatukosesha amani,
Magonjwa haya Hatari.

Homa inavyouguza, joto kutupa mwilini,
Puresha inaongeza, inafika kileleni,
Pima joto husikiza, jibu lake ndiyo gani,
Magonjwa ni hatari.

Mafua nawaeleza, yaonekana puani,
Hili la kuambukiza, awe nani ama nani,
Kamasi hujitokeza, hata kuumwa kichwani,
Magonjwa ni hatari.

Na kikohozi chunguza, hutokea mdomoni,
Rangi yake huchukiza, nyeupe hata kijani,
Mgonjwa hujikohoza, kuondoa kifuani,
Magonjwa ni hatari.

Vipele navyo humiza, viruturutu ngozini,
Haiwezi kukwambiza, ndugu yangu samahani,

Huwasha na kuvijaza, usaha hadi pomoni,
Magonjwa ni hatari.

Ukimwi hautaweza, ni ugonjwa namba wani,
Wale wasiosikiza, hujutia ni kwa nini?,
Mwendo mbaya hukataza, nasihi badilikeni,
Magonjwa ni hatari.

Malaria naongeza, m'mbu  atutakiani?,
Na damu hutumaliza, kwa kufyonza kinywani,
Homa kali hutokeza, kutuacha nukusani,
Magonjwa ni hatari.

Na kichocho sitasaza, unatokea majini,
Konokono hueneza, hili ninawajuzeni,
Hata damu hutokeza, unapoenda uani,
Magonjwa ni hatari.

Kifafa ewe sikiza, hushtusha wajameni,
Mja ninajiuliza, mbona kaumba Rabani?,
Kwanguka kwa kujikaza, unazirai pu! Chini,
Magonjwa ni hatari.

Ukoma huambukiza, si salama asilani,
Vidole hujilegeza, na kukatika jamani,
Mishipa huutatiza, ya ufahamu bongoni,
Magonjwa ni hatari.

Mwishoni sitaongeza, naomba tutahadharini,
Wengi tumewapoteza, wamesafiri mbinguni,
Magonjwa nasisitiza, naomba tujichungeni,
Magonjwa ni hatari.

**JITATHMINI**

1. Shairi hili lina mishororo mingapi?
2. Mshororo wa pili katika shairi huitwaje?
3. Stadi wa kuyaghani mashairi huitwaje?
4. Taja magonjwa mawili kupitia kwa shairi hili na utoe madhara yao.
5. Shairi lenye kufupishwa kibwagizo linaitwaje?

**UMOJA NI NGUVU.**
**Mtunzi: Alfred Lobawoi**
**Lakabu: Malenga Mweledi Chipukizi**
**Gatuzi : Turkana**

Yalisemwa na wahenga, leo ninaweka sawa,
Maji sitozidi unga, niwapikie ubwabwa,
Ni maana ninalenga, mkapate kuyajuwa,
Umoja kutia nguvu, kutengana udhaifu.

Mkono tukiuunga, mambo bora yanakuwa,
Kisumu na Lungalunga, na mandugu tutakuwa,
Hakuna vita vya panga, hili naomba tambuwa,
Umoja kutia nguvu, kutengana udhaifu.

Kama nyuki kwa mzinga, mchango wote watowa,
Maji hata na mchanga, mzingani wanatowa,
Asali wanaipanga, za akiba na kuliwa,
Umoja kutia nguvu, kutengana udhaifu.

Jiwe haliwezi jenga, bali ni mawe ndo huwa,
Moja huwezi kuunga, ni mengine hutumiwa,
Mjenzi hawezi jenga, bila ya kusaidiwa,
Umoja kutia nguvu, kutengana udhaifu.

Mwanawe kuengaenga, athari huchukuliwa,
Wazazi wote waunga, mwana anapozaliwa,

Kutokana na ujinga, hadi werevu kukuwa,
Umoja kutia nguvu, kutengana udhaifu.

Darasani nawe chunga, pweke huwezi elewa,
Nenda kwa wengine changa, jibu nalo utapewa,
Kuuliza si ujinga, kutouliza ndo huwa,
Umoja kutia nguvu, kutengana udhaifu.

Bidii kama ya mhanga, maishani yatakiwa,
Angavu uwe ja anga, ung'ae tena ja juwa,
Ufuatapo kuchanga, mwisho utafanikiwa,
Umoja kutia nguvu, kutengana udhaifu.

**JITATHMINI**

1. Shairi ulilosoma ni la aina gani?
2. Mwanzo katika ubeti wa pili ni upi?
3. Kupitia kwenye ubeti wa tatu, Bidii za nyuki zaweza kulinganishwa na nani?
4. Taja methali moja inayohusiana na shairi hili.
5. Mhanga ni nani?

**MAJINA YA MISIMU**
**Mtunzi: Christopher Musa Kalunda**
**Lakabu: Malenga Mwepesi**
**Gatuzi : Vihiga**

Somo nanga limeng'oa, masikizi weka wazi,
Chondechonde limatia, myashike waziwazi,
Ni bora kuyatumia, Kiswahili kiwe ngazi,
Ni majina ya misimu, tuyatiye akilini.

Misimu pia majira, kwa mwaka hubadilika,
Mifano yake ni bora, shika kalamu andika,
Joto jingi ni majira, ambayo huitwa chaka,
Ni majina ya misimu, tuyatiye akilini.

Kifuku au masika, mvua nyingi kwa mwaka,
Mkaragazo hakika, hunya kwa fujo kifika,
Vuli,mchoo andika, mvua fupi kwa mwaka,
Ni majina ya misimu, tuyatiye akilini.

Pia huja kiangazi, majira ya jua kali,
Ukame ni waziwazi, maji kupata ni fali,
Na yakaja mazigazi, maji yasiyo ya kweli,
Ni majina ya misimu, tuyatiye akilini.

Kipupwe nawajuzeni, ni baridi na upepo,
Mapukutiko juweni, miti majani hayapo,

Machipuko fahamuni, ndipo majani yajapo,
Ni majina ya misimu, tuyatiye akilini.

Pepo nazo maizini, kila upande huvuma,
Kuna ule wa kusini, huitwa KUSI kivuma,
Nao wa kaskazini, KASKAZI mmesoma,
Ni majina ya misimu, tuyatiye akilini.

Matlai ni msimu, upepo wa mashariki,
Wa magharibi yahom, huvuma nao mkiki,
Kikukusi mfahamu, hung'oa hata visiki,
Ni majina ya misimu, tuyatiye akilini.

Somo kikomo natia, majina ni mengi sana,
Na lugha bora tumia, misimu kitajiana,
Kiswahili tafitia, na mageni kufunzana,
Ni majina ya misimu, tuyatiye akilini.

**JITATHMINI**

1.Kitabu cha mashairi huitwaje?
2.Utao wa mleo katika ubeti wa kwanza ni
3.Shairi lenye mishororo miwili katika kila ubeti linaitwaje?
4.Misimu ina kisawe chake ni
5.Kipupwe ni kwa baridi shadidi kama vile ________ni kwa joto jingi.

**NAWEZA FANYA LOLOTE**
**Mtunzi: Christopher Musa Kalunda**
**Lakabu: Malenga Mwepesi**
**Gatuzi : Vihiga**

Jina langu ni Akiru, kipusa Mturkana,
Mvua ndiyo 'akiru,' nipopata langu jina,
Bila shaka nipo huru, kupa moyo wasichana,
Akiru ninajipenda, naweza fanya lolote.

Naweza fanya lolote, katu sinibagueni,
Tuliumbwa sawa sote, hili nalo maizini,
Kiume na kike kote, mfinyanzi ni Manani,
Akiru ninajipenda, naweza fanya lolote.

Elimu inanifaa, kama yule mvulana,
Kwayo nitajiandaa, maishani kupambana,
Neza kuwa injinia, au mhunzi kasana,
Akiru ninajipenda, naweza fanya lolote.

Uhuru wa kuamua, wavyele msininyime,
'Keketaji kikataa, niruhusu niyateme,
Ndoa za mapema pia, moto huo tuuzime,
Akiru ninajipenda, naweza fanya lolote.

Kazi bora yanifaa, vyeti vyangu nikitoa,
Si sawa kunibagua, kwa hino kike jinsia,

Mradi gange kujua, nitaifanya kwa nia,
Akiru ninajipenda, naweza fanya lolote.

Na mitego ya dunia, ya 'mafisi' kunijia,
Kwa urongo na hadaa, kiwapa wanapotea,
Ni bora kujilindia, asali kuhifadhia,
Akiru ninajipenda, naweza fanya lolote.

Sura yangu yapendeza, na mwili wangu wa Mola,
Hakika sitajibeza, na kujiona jalala,
Mambo mengi nayaweza, kuyafanya bila hila,
Akiru ninajipenda, naweza fanya lolote.

Ubeti wa nane huu, ushauri nawapeni,
Mabinti sijisahau, na kujitweza moyoni,
Jiwekeni pale juu, nao moyo jitieni,
Akiru ninajipenda, naweza fanya lolote.

**JITATHMINI**

1.Ni nini maana ya Jina *akiru* kulingana na ubeti wa kwanza?
2.Akiru anadai kutobaguliwa kwa misingi ipi?
3.Shairi hili lina mishororo mingapi?
4.Ubeti wa nne una ujumbe gani kwa wasichana?
5.Mleo wa ubeti wa pili una mizani mingapi?
6.Eleza maana ya; Kujitweza moyoni, Ukeketaji na Mhunzi

**MICHEZO**
**Mtunzi: Christopher Musa Kalunda**
**Lakabu: Malenga Mwepesi**
**Gatuzi :Vihiga**

Kitabu weka mezani, na kalamu mkononi,
Na makini sikizeni, somo letu darasani,
Mifano nitawapeni, iwafae maishani,
Ni aina ya michezo, bora nyinyi kufaidi.

Ugani ukiingia, riadha ni furufu,
Mfano kuogelea, na mbio zinazokifu,
Kuruka na kutembea, magalacha tukisifu,
Ni aina ya michezo, bora nyinyi kufaidi.

Kabumbu au kandanda, chezea yako miguu,
Kipute,soka kipenda, utaje mchezo huu,
Wengi kote huupenda, kushabikia falau,
Ni aina ya michezo, bora nyinyi kufaidi.

Jugwe tia akilini, ni wa kamba kuvutana,
Judo nao wapinzani, chini wanaangushana,
Kibemasa kwa wandani, ni raha kutafutana,
Ni aina ya michezo, bora nyinyi kufaidi.

Masumbwi pia makonde, mchezo wa kupigana,
Saratanji usikonde, ni chesi kuchezeshana,

Nage pia uupende, vibao saba panguana,
Ni aina ya michezo, bora nyinyi kufaidi.

Mazoezi ya viungo, ugani huitwa kwata,
Na mpira wa magongo, gonga kwa gongo kipata,
Raga nao si urongo, toka shoti kiupata,
Ni aina ya michezo, bora nyinyi kufaidi.

Mpira wa pete nao, pete ndani hupitia,
Wa vikapu angalao, mpira wako dundia,
Usisahau wa bao, namu na kete tumia,
Ni aina ya michezo, bora nyinyi kufaidi.

Kaditama nakomea, ni mingi sitamaliza,
Michezo karamkia, afya zetu kuzikuza,
Mili na akili pia, michezo yetu hukuza,
Ni aina ya michezo, bora nyinyi kufaidi.

**JITATHMINI**

1.Andika kichwa mwafaka cha shairi hili.
2.Shairi hili lina beti ngapi?
3.Taja shairi hili ni la aina gani?
4.Mwandishi ametaja aina ngapi ya michezo?
5.Eleza maana ya maneno yafuatayo; Magalacha, Saratanji na Toka shoti

**AINA ZA USHURU**
**Mtunzi: Christopher Musa Kalunda**
**Lakabu: Malenga Mwepesi**
**Gatuzi :Vihiga**

Kodi kipenda ushuru, kwa serikali yatupasa,
Chanzo kuu cha mapato, kwa serikali ya sasa,
Bora sisi kwajibika, kulipa pasi kukosa,
Ni aina za ushuru, wananchi jifunzeni.

Na kodi nchini Kenya, pana makundi mawili,
Kilipa moja kwa moja, ni bayana na dhahili,
Pili ni iso dhahiri, kinunua kihalali,
Ni aina za ushuru, wananchi jifunzeni.

Wakazi wote nchini, hata wale wagenetu,
Sote kodi ya mapato, inatufaradhi kwetu,
Mifano yetu ni chekwa, kulipa ni wajibetu,
Ni aina za ushuru, wananchi jifunzeni.

Na kodi ya Mashirika, haki yenu kujuweni,
Inalipwa na kampuni, kwa mapato ya mwakani,
Zetu zote na kigeni, asilimia hupani,
Ni aina za ushuru, wananchi jifunzeni.

Kulingana na mapato, tarehe kenda mwezini,
Kwa chake hicho kiwango, mwajiriwa alipani,

Mwajiri huwajibika, kwa watoza shirikani,
Ni aina za ushuru, wananchi jifunzeni.

Pia kodi ya bidhaa, ni muhimu kujuweni,
Hulipwa kwazo bidhaa, zizalishwazo nchini,
Pia ushuru hutozwa, kwa bidhaa za kigeni,
Ni aina za ushuru, wananchi jifunzeni.

Kaditama natimia, kodi zetu tulipeni,
Sheria zetu za nchi, ni bora tufuateni,
Yakawa maendeleo, ya kwetu sisi nchini,
Ni aina za ushuru, wananchi jifumzeni.

**JITATHMINI**

1.Shairi hili lina beti ngapi?
2.Taja aina tatu za ushuru zilizotajwa shairini.
3.Eleza ujumbe unaojitokeza katika ubeti wa mwisho.
4.Shairi hili ni la aina gani?
5.Eleza maana ya maneno haya; Arudhi, Mghani na Ushuru.

**NAIONEA FAHARI**
**Mtunzi: Ali M. Mwanza**
**Lakabu: Malenga Kande**
**Gatuzi : Kwale**

Bendera ya nchi yangu, ni nzuri inapendeza,
Iwapo machoni mwangu, haiwezi nichukiza,
Huliwaza moyo wangu, kwa rangize zapendeza,
Naionea fahari, bendera yetu ya Kenya.

Ianzayo ni nyeusi, rangi ninayojivuna,
Ndimi Mkenya halisi, napendeza kiniona,
Ninaupenda weusi, rangi yetu kila kona,
Naionea fahari, bendera yetu ya Kenya.

Nyeupe ni ya amani, itawale Kenya nzima,
Itutawale nyoyoni, amani yenye heshima,
Siturudishe vitani, tukaonwa kama kima,
Naionea fahari, bendera yetu ya Kenya.

Nyekundu ni damu yetu, ilomwagika vitani,
Yao mashujaa wetu, kuitafuta amani,
Nasi tuwe nao utu, kuishi nao nyoyoni,
Naionea fahari, bendera yetu ya Kenya .

Kijani ni nchi yetu, tuliyojinyakulia,
Ilojaa mali zetu, zilizojinawiria,
Yakawa mavuno yetu, tulipokoma kulia,
Naionea fahari, bendera yetu ya Kenya.

Na kinga yetu ni ngao, ndo utamaduni wetu,
Tulojikingia hao, walo maadui wetu,
Ukapiku ala zao, tukapewa nchi yetu,
Naionea fahari, bendera yetu ya Kenya.

Mkuki yetu risasi, tulipokuwa vitani,
Vita vya watu weusi, kuitafuta amani,
Kawajaza wasiwasi, wakawa bila amani,
Naionea fahari, bendera yetu ya Kenya.

Mwisho ninatoa wito, wito huno sipuuze,
Tuifanye iwe kito, cha thamani kwa rangize,
Tuipake manukato, kileleni tupandize,
Naionea fahari, bendera yetu ya Kenya.

**JITATHMINI**

**1.** Kwa kuzingatia vina vya kati na vya mwisho, shairi hili ni la aina gani?

2. Mshororo wa mwisho wa shairi hili ni wa aina gani?

3. Vina vya kati na vya mwisho vya ubwti wa tatu ni gani?

4. Rangi nyeusi kwenye bendera ya Kenya huashishiria nini kulingana na mshairi?

5. ________________________________ni rangi, inayoashiria damu ya Mashujaa kwenye bendera ya Kenya.

## MATUNDA NA MIMEA

**Mtunzi: Ali M. Mwanza**
**Lakabu: Malenga Kande**
**Gatuzi : Kwale.**

Parachichi najijua, mwenye nayo kokwa ndani,
Punde unaponigua, nyama yangu i kijani,
Ni tamu kama halua, na ladha ilo laini,
Parachichi ndimi mwana, mamangu mparachichi.

Embe nami najitosa, nachangia mkutano,
Kokwa siwezi ikosa, kiiva niko manjano,
Nina ladha tamu hasa, nyama ilo lainino,
Embe ni tamu kiiva, mamangu huwa ni mwembe.

Wanijua stafeli, japokuwa si kurutu,
Wa ladha tamu asali, na ngozi yenye vidutu,
Ndani mbegu kizimwili, weupe wapenda watu,
Stafeli najivuna, mamangu mstafeli.

Na mimi hapa zabibu, mdogo wa langu umbo,
Shambani ndimi katibu, zambarau ndilo pambo,
Mivinyoni ni karibu, utomwili kwenu tambo,
Zabibu nafurahia, mamangu ni mzabibu.

Sitakishindwa tufaha, tunda nilo majimaji,
Niivapo ni furaha, wekundu ni kwa mlaji,
Ni tamu mie tufaha, atajiramba mlaji,
Endapo mie ndo mwana, mamangu ni mtufaha.

Fenesi ninasogea, harufu tele puani,
Ladha tamu kuwapea, nazo kokwa nyingi ndani,
Ni kijani kuonea, na vidutu ki mibani,
Kisha humea mtini, mti ni wa mfenesi.

Nami ndizi meniona? Izu ndimi kwa wengini,
Ninapendwa kila kona, ninamea mkunguni,
Kiiva niko manjana, utamu u haluani,
Niko tamu sijigambi, mama yangu ni mgomba.

Nami chungwa mwanachani, niivapo ni manjano,
Danzi naye namwigani, chenza naye kwa muswano,
Siponigua makini, nakuliza ndo mfano,
Huzaliwa mviringo, mama yangu ni mchungwa.

Taniwachaje tomoko, kutoingia kapuni,
Nikujaze furahiko, kinitia mdomoni,
Vidutu vyenye mipako, na kokwa nyeusi ndani,
Nyama yangu ni nyeupe, lonizaa mtomoko.

Nilitagiwa mibani, huwa mkubwa si haba,
Na kitita kileleni, na ganda ni mibamiba,
Umbo ni kama yaini, kinidhuru nakukaba,
Basi ndo mimi nanasi, huzawa na mnanasi.

Papai nimeshafika, nilo wazi mwangu ndani,
Utomvu kijeruhika, mweupe na tumba ndani,
Kiiva utatosheka, kwa ladha tamu laini,

Nyama yangu ni laini, mamangu ni mpapai.

**JITATHMINI**

1. Taja matunda matatu yaliyotajwa kwenye shairi
2. Ni tunda lipi lenye kokwa nyeusi ndani, vidutu kwenye ganda na nyama nyeupe
3. Kulingana na ndizi, inamea________________________________
4. Ni tunda lipi linapoiva hubaki rangi ya kijani kwa mujibu wa shairi?
5. Parachichi linaposema 'Punde unaponigua' linamaanisha kuwa ______________________________________________

**HAKI ZA WATOTO**
**Mtunzi: Lilian Alividza**
**Lakabu: Malkia wa Nyikani**
**Gatuzi : Kakamega**

Watoto wanayo haki, wana haki ya kupendwa,
Hakii ya kushiriki, mema jamani hupandwa,
Tusijewafunza chuki, uhayawani kutendwa,
Watoto wanayo haki, tuwafunze haki zao.

Haki kupata elimu, kuingia skulini,
Wajifunze ya muhimu, wana watoke kizani,
Haitekeki elimu, ilimu ina thamani,
Watoto wanayo haki, tuwafunze haki zao.

Wana haki ya kuishi, kupata malezi mema,
Mazingiraa wahshi, yanachangia dhuluma,
Tuwache pia uzushi, watoto wawe salama,
Watoto wanayo haki, tuwafunze haki zao.
Akilini unakili, haki ya kuendelezwa,
Tuwafunze maadili, muhimu kusikilizwa,
Wakamjue Jalali, haramu kugandamizwa,
Watoto wanayo haki, tuwafunze haki zao.

Haki ya kulindwa kweli, wasitendewe maovu,
Tuzuie ukatili, vitendo vile viovu,
Tuwalinde lama dali, tusiwape maumivu,

Watoto wanayo haki, tuwafunze haki zao.

Wasitelekezwe katu, wapewe mwema mwongozo,
Pia yatima ni watu, tusiwe wenyee bezo,
Ushamiri pia utu, mzazi ni sheshe nguzo,
Watoto wanayo haki, tuwafunze haki zao.

Mwana haitaji kazi, usiajiri mtoto,
Tena za sulubu kazi, twawabebesha mazito,
Hawahitaji ghawazi, uikuze yao ndoto,
Watoto wanayo haki, tuwafunze haki zao.

Asibaguliwe mwana, apewe huduma bora,
Walemavu pia wana, gashi sipashwe tohara,
Fahamu wana ni wana, tajiri pia fukara,
Watoto wanayo haki, tuwafunze haki zao.

**JITATHMINI**

1)Taja mleo wa ubeti wa tano.
2)Taja mkarara wa shairi hili.
3)Shairi hili lina idadi ya silabi ngapi?
4) taja bahari ya shairi hili
5)Aliye na uwezo wa kutunga shairi

**MWANAGENZI HASANATI**
**Mtunzi: Lilian Alividza**
**Lakabu: Malkia wa Nyikani**
**Gatuzi: Kakamega**

Nakusihi mwanagenzi, koma wako utundu,
Utundu kwa mwanafunzi, haramu siwe mtundu,
Huadhibu mkufunzi, mwana akiwa mtundu,
Uzingatie nidhamu, usije katu ukajuta.

Mtoto mwenye heshima, huepuka sana ghamu,
Kamwe usiwe dhalimu, watazani chakaramu,
Mwana siwe bahaimu, utakuja jilaumu,
Uzingatie nidhamu, usije katu ukajuta.

Uwe mwenye tabasuri, mwana uliye hariri,
Ufanye nawe firari, wasidhani u hakiri,
Jambo la mana busuri, mwanagenzi fanya ari,
Uzingatie nidhamu, usije katu ukajuta.

Siwe mwenye kughilibu, ukatuletea gubu,
Huluka iwe ajibu, usiwe mwenye ghadhabu,
Mwana aliye adibu, huepuka masaibu,
Uzingatie nidhamu, usije katu ukajuta.

Darasani usigonezi, utabaki kuwa bozi,
Silaha yako ya ghazi, ni kalamu umaizi,

Ujinga ni banguzi, ukatae waziwazi,
Uzingatiie nidhamu, usije katu ukajuta.

Ngangana uwe fahali, sionekane dhalili,
Masomoni siwe dhuli, mtihani ukafeli,
Tena fanya fulifuli, uwe mtoto aali,
Uzingatie nidhamu, usije katu ukajuta.

Nimekwishafika dali, usizembe bilikuli,
Yawe sheshe maadili, ufaulu kule skuli,
Kila siku usali, akuongoze Jalali,
Uzingatie nidhamu, usije katu ukajuta.

**JITATHMINI**

1)Shairi hili ni la aina gani?
2)Shairi hili lina beti ngapi?
3)Taja idadi ya mishororo katika shairi hili
4)Taja vina vya kati na vya mwisho katika ubeti wa nne.
5)utaje ukwapi wa mshororo wa kwanza ubeti wa tatu.

**UKABILA NI ADUI**
**Mtunzi: Lilian Alividza**
**Lakabu: Malkia wa Nyikani**
**Gatuzi :Kakamega**

Ukabila jinamizi, umezagaa ntini,
Umeleta ubaguzi, watukosesha amani,
Kule kwenye makaazi, sasa tumo hatarini,
Ukabila sumu kali, yaua wetu umoja.

Ukitafuta huduma, unaulizwa kabila,
Ukabila kama homa, menea kila pahala,
Husababisha husuma, twaitana gulagula,
Ukabila sumu kali, yaua wetu umoja.

Wengi mekosa ajira, sababu ya ukabila,
Huzidisha ufukara, ukabila ni ja jela,
Huleta tele madhara, twangamize ukabila,
Ukabila sumu kali, wyaua wetu umoja.

Huzua belele chuki, inaleta utengano,
Utoeka urafiki, hayaishi malumbabano,
Ya ukabila hamaki, huleta mafarakano,
Ukabila sumu kali, yaua wetu umoja.

Hadi ndani ya siasa, ukabila hutokeza,
Ukabila watutesa, tena watugandamiza,

Tumeshakosa hamasa, tunaishi kwenye kiza,
Ukabila sumu kali, yaua wetu umoja.

Toka bara lama pwani ,ukabila angamiza,
Watufanya waja duni, jahara watuumiza,
Ndugu zangu amkeni, msiwe tu mwanyamaza,
Ukabila sumu kali, yaua wetu umoja.

Wakenya sisi ni ndugu, mama yetu huyu kenya,
Tunakataa vurugu, wakabila twawaonya,
Tunapanda nzuri mbegu, Latifu ilinde Kenya,
Ukabila sumu kali, yaua wetu umoja.

**JITATHMINI**

1)Eleza umuhimu wa kichwa cha shairi?
2Tofautisha kati ya mshororo na ubeti?
3)Tarbia ni shairi la mishororo mingapi?
4)mshororo wa kwanza katika ubeti huitwaje?
5)tofautisha kati ya mloto na mleo?

## VIUNGO VYA MWILI
**Mtunzi: Lilian Alividza**
**Lakabu: Malkia wa Nyikani**
**Gatuzi: Kakamega**

Figo nacho ni kiungo, kinachosafisha damu,
Umbo la hiki kiungo, ni ja haragwe fahamu,
Viungo ni muhimu, mwilini mwanadamu,
Taratibu mwanagenzi, jua viungo vya mwili.

Na hapa pa kitefute, ni mshipa wa shavuni,
Katu nyongo usitete, yeshusha mlo tumboni,
Pafu usisitesite, safisha hewa mwilini,
Taratibu mwanagenzi, jua viungo vya mwili.

Ishikiliayo meno, hino nyama ni gani,
Eti mwataka mfano, mnakili akilini,
Tukaandike kwa wino, ni ufizi sikizeni,
Taratibu mwanagenzi, jua viungo vya mwili.

Watoto mikono hewani, mkono pia kiungo,
Kinatokea begani, tia kwenye bongo,
Shika kitu mkononi, kazi ya hicho kiungo,
Taratibu mwanagenzi, jua viungo vya mwili.

Twendelee wanafunzi, utaya kwenye mabano,
Ni mfupa wanagenzi, ushikiliayo meno,

Ninalonga wanagenzi, mkaache minongono,
Taratibu mwanagenzi, jua viungo vya mwili.

Yakiwa mengi ni meno, twatafunia chakula,
Kwa umoja sema jino,usiwe gulagula
Hupigwa mswaki meno, ukishamaliza kula,
Taratibu mwanagenzi, jua viungo vya mwili.

Moyo ukipenda mtima,kinafanya kazi gani?
Twangazie kwa hikima, eti kinasukuma nini?
Damu kinaasukuma, ikaenee mwilini,
Taratibu mwanagenzi, jua viungo vya mwili.

Nikweleze ya kibofu, mtoto uwe makini,
Usijitie udufu, chapatikana tumboni,
Ni kifuko acha hofu, ni cha mkojo yakini,
Taratibu mwanagenzi, jua viungo vya mwili.

Pasi kuwa na ulimi, tungeonja mlo vipi?
Kuelimisha sikomi, twajua ladha ya pipi,
Asante sana ulimi, kutamka siogopi,
Taratibu mwanagenzi, jua viungo vya mwili.

Pasi kuwa na miguu, vipi ungelitembea,
Ja gurudumu mguu, kotekote twatembea,
Huwa miwili miguu, kwa binadamu tambua,
Taratibu mwanagenzi, jua viungo vya mwili.

**JITATHMINI**

1)Eleza umuhimu wa viungo vifuatavyo: Ufizi, pafu, Nyongo, Figo

2)Tofautisha kati ya ukwapi na utao?

3)Ubeti wa tano una mishani ngapi katika kila mshororo,

4)Shairi hili lina beti ngapi?

5)Mshipa wa shavuni huitwaje?

**TULIA BINTI**
**Mtunzi: Lilian Alividza**
**Lakabu: Malkia wa Nyikani**
**Gatuzi: Kakamega**

Zamu yako msichana, nikupe sheshe nasaha,
Uwe insi mwanana, alo na nyota ya jaha,
Acha kupiga ubwana, utaumia wadhiha,
Tulia binti tulia, usije ukapotoka.

Usifanye stihizai, masomoni fanya ari,
Na uongo ni adui, takutia taksiri,
Kote utapigwa zii, ukiwa mwana jauri,
Tulia binti tulia, usije ukapotoka.

Utageuka kinyago, masomo ukiyaasi,
Sijibandike mzigo, soma unayo nafasi,
Watakutwika magogo, dunia bahari tesi,
Tulia binti tulia, usije ukapotoka.

Mwana jifunge masombo, hujatosha kuwa mama,
Jijenge siende kombo, uwe mwana wa heshima,
Wenye ulimi ulimbo, chunga hawana huruma,
Tulia binti tulia, usije ukapotoka.

Sijitie ushaibu, kusikiza wenye hila,
Na utashikwa sharubu, utakandikwa bakora,

Ushike yako adabu, ya vuta kheri subira,
Tulia binti tulia, usije ukapotoka.

Ujue mbichi na mbivu, umuhimu wa madili,
Gashi uwe mtulivu, tena vuta taamuli,
Kitaka kuwa mwerevu, utuze yako akili,
Tulia binti tulia, usije ukapotoka.

Utunge na kutungua, usijevuliwa mbeko,
Ukache kujifutua, ovyo kupiga kidoko,
Utondozi natondoa, epuka wa roho choko,
Tulia binti tulia, usije ukapotoka.

**JITATHMINI**

1)Shairi hili lina vipande vingapi
2) Shairi hili lina ni la aina gani?
3)Lipe shairi hili kichwa kingine ?
4)Mshororo wa mwisho katika kila ubeti unaodiwarudiwa waitwaje?
5)Utaje utao wa mshororo wa kwanza ubeti wa tatu?

**UKULIMA NDIYO KAZI**
**Mtunzi: Kaka Fred**
**Lakabu: Malenga wa Dhahabu**
**Gatuzi : Bungoma**

Ukulima ndiyo kazi, enyi nyote mjueni,
Mgundani ndiyo zizi, jembe ninalo begani,
Siutaki upuuzi, ofisi yangu shambani,
Ukulima ndiyo kazi, inayonipa riziki,

Kilimo ndicho kiini, uchochole ondokea,
Uchumi inueneni, maisha kuendelea,
Tuepuke uzembeni, maghala yetu kujaa,
Ukulima ndiyo kazi, inayonipa riziki,

Tuache vinenoneno, ukulima ubaini,
Tukamate misumeno, tuende sote kondeni,
Kataa tena maneno, uvivu epuukeni,
Ukulima ndiyo kazi, inayonipa riziki,

Tukuze mazao yetu, Tuepuke hili jaa,
Tuungane Kenya yetu, natoa wangu wosia,
Maendeleo ni kwetu, asiyetaka ana udhia,
Ukulima ndiyo kazi, inayonipa riziki,

Ufukoni nimefika, nimekupa hii Siri,
Niite nitaitika, watakao mashauri,
Machache nimeandika, naomba utie ari,

Ukulima ndiyo kazi, inayonipa riziki,

**JITATHMINI**

1. Mwandishi anatuhimiza tufanye nini?
2. Kariri kibwagizo cha shairi hili.
3. Je, ukulima una umuhimu wowote?
4. Shairi hili lina beti ngapi?
5. Kwa kutumia kamusi yako, eleza maana ya maneno yafuatayo; Mgunda, uchochole, maghala.

**TUKIENZI KISWAHILI**
**Mtunzi: Kaka Fred**
**Lakabu: Malenga wa Dhahabu**
**Gatuzi :Bungoma**

Nasimama kwa imara, nieleze mlo nyuma,
Sielezi kwa papara, si wazimu nayosema,
Sielezi kwa ukora, sijelipa kwa kuvuma
Tukienzi Kiswahili, dhahabu ya lugha yetu,

Lugha hii ndiyo bora, kama titi lake mama,
Yasifika kwa ubora, toka bara hadi bama,
Uchumi na biashara, vimekuwa vyote wima,
Tukienzi Kiswahili, dhahabu ya lugha yetu,

Umoja ndio imara, mawasiliano mema,
Lugha hii ndiyo bora, ndiyo chanzo kwayo mema,
Kiswahili kinang'ara, tujikaze kujituma,
Tukienzi Kiswahili, dhahabu ya lugha yetu,

Hadi tama nafikia, wino wangu naachia,
Mwisho nasisitizia, Kiswahili endelea,
Hivyo utajivunia, uzuri huu kwa kina,
Tukienzi Kiswahili, dhahabu ya lugha yetu,

**JITATHMINI**

1. Mwandishi anatusisitizia nini ?
2. Eleza namna Kiswahili kilivyoimarisha uchumi.

3. Shairi hili lina mizani mingapi kwa jumla?
4. Eleza maana ya papara,
5. Taja taifa lililotajwa kwenye shairi hili.

**MZALENDO MIMI.**
**Mtunzi: VINCENT IMBALI**
**Lakabu: Malenga mwona mbali**
**Gatuzi: Vihiga**

MZALENDO: Nakusihi mwenzangu, nisikize kwa makini.
Kupenda nchi yangu, kwatoka kwangu moyoni.
Mbona wewe mwenzangu, hutaki hili kubaini?

VUGUVUGU: Nchi imekupa nini, ndipo upate kupenda?
Hali kwako kiamboni, unaishi kwa mabanda.
Ukifilia shambani, kwa kazi kama punda?

MZALENDO: Vuguvugu nisikize, mja akiwa shambani.
Mbona hilo likulize, na kukunyima amani?
Wapenda ujilegeze, kizembe huko nyumbani?

VUGUVUGU: Nchi hii haijali, kuniona masikini.
Wakuu wa serikali, watuchekea enzini.
Wakifyonza zetu mali, kutuacha taabani.

MZALENDO: Ni wewe wa kulaumu, kwa kuwaweka enzini.
Kura yako ufahamu, ulitia chaguzini.
Kama 'lichagua sumu, huondoki lawamani.

VUGUVUGU: Kwa majasho ujenzini,yanamwagika usoni.

Hata kule viwandani, tunajituma kazini.
Malipo nayo ni duni, yanatufinyia chini.

MZALENDO: Do! Aliyewapa kiti, ndiye alokupa kumbi.
Kwa bidii jizatiti, utaacha kula vumbi.
Na usiwe msaliti, ujue hilo ni dhambi.

VUGUVUGU: Matongo umenitoa, yaliyokuwa machoni.
Hivi sasa nimejua, nina wajibu nchini.
Ufanisi kufikia, bidii iwe kazini.

MZALENDO: Nafurahi kusikia, ‘mewacha kiburi chako.
Kwamba utajitolea, kuboresha nchi yako.
Kilele tutafikia, tukianzia huko kwako.

PAMOJA: Hapa ndipo tunatua, kwa pamoja tumejua.
Nchi haiwezi kua, bila idili kujua.
Pendo tutapalilia, uzuri tupate jua.
Wazalendo tutasimama, tuiweke Kenya mbele.

**JITATHMINI.**

1. Shairi hili ni la aina gani?
2. Toa sababu tatu zinazomfanya Vuguvugu asipende nchi yake.
3. Siku ya uchaguzi, kitu gani hufanyika?
4. Taja methali iliyotumika katika shairi hili.
5. Mzalendo ni mtu anayeipenda nchi yake. Je, asiyeipenda nchi yake huitwa?

**TULIPE USHURU.**
**Mtunzi: Vincent Imbali.**
**Lakabu: Malenga mwona mbali.**
**Gatuzi** : **Vihiga**.

Nimekuja ukumbini,
Niwaambie ya muhimu,
Hivyo naomba nisikilizeni,
Ili mpate huu ufahamu,
Kulipa ushuru wa nchi,
Heko kwa waliobaini.

Ushuru wa serikali,
Ni malipo yenye faida,
Huisongeza nchi mbali,
Na kuiondolea nyingi shida,
Kulipa ushuru wa nchi,
Heko kwa waliobaini.

Elimu hufaidika,
Kutokana na ushuru,
Madarasa yakajengeka,
Wanafunzi wakashukuru,
Kulipa ushuru wa nchi,
Heko kwa waliobaini.

Maafisa huongezeka,

Ushuru tukiulipa,
Usalama wataweka,
Tuishi bila kupapa,
Kulipa ushuru wa nchi,
Heko kwa waliobaini.

Hizi reli za kisasa,
Zaendelezwa kwa ushuru,
Angatua na njia za kisasa,
Zinapambwa kwa ushuru,
Kulipa ushuru wa nchi,
Heko kwa waliobaini.

Ili kusambaza umeme,
Na maji ya kutufaa,
Ushuru wetu tuutume,
Bila visababu kutoa,
Kulipa ushuru wa nchi,
Heko kwa waliobaini.

Naumaliza mtungo,
Nikiwahusia wazalendo,
Sote tuweke mipango,
Ya kujenga nchi kwa vitendo,
Tulipe ushuru wa nchi,
Ufanisi tuufikie.

**JITATHMINI**

1. Taja faida zozote tano zinazoletwa na kulipa ushuru.
2. Kulingana na shairi hili, ushuru hulipwa kwa nani?
3. Taja pembejeo mbili wanazohitaji wakulima ili kuendeleza kilimo.
4. Eleza ujumbe unaojitokeza katika ubeti wa tano.
5. Kulingana na ubeti wa sita, maafisa wakiongezeka kitu gani hufanyika?
6. Ubeti wa pili una mizani mingapi?

**WAZALENDO**
**Mtunzi: Mwl Vincent Imbali**
**Lakabu: Malenga mwona mbali**
**Gatuzi: Vihiga**

Sisi sote ni wakenya, na Kenya ni yetu sote,
Nauliza kina nyanya, nanyi wazalendo wote,
Kwa nini mnatusinya, kwa kutemeana mate?
Wazalendo kupendana, huo ndio uungwana.

Damu yake Wabukhala, ni kama yake Katana,
Na akili za Omalla, zafikiri kama za Zuena,
Hili na hilo kabila, mahitaji yafanana,
Wazalendo kupendana, huo ndio uungwana.

Jalali alituumba, wanadamu kiufundi,
Kwa kweli alituumba, tofauti nao bundi,
Tuzidi huko kutamba, tutembee kwa vikundi,
Wazalendo kupendana, huo ndio uungwana.

Tukitaka kwenda mbali, naliweka waziwazi,
Tukatae kwa ukali, ujinga wa ubaguzi,
Pendo liwe mhimili, na lifundishwe vizazi,
Wazalendo kupendana, huo ndio uungwana.

Magaidi watakoma, si sote tukiungana,
Tutaishi bila lalama, na mabaya kuelezana,

Utadumu usalama, jirani tukijuana,
Wazalendo kupendana, huo ndio uungwana.

Kilimo kitatukuka, sote tukiwa pamoja,
Biashara zitashika, na kufikia wateja,
Elimu taimarika, afya na mali ya waja,
Wazalendo kupendana, huo ndio uungwana.

Yangu habari nakoma, ninatua ukingoni,
Hili jambo nalisema, mjini na vijijini,
Wakenya tukae wima, wa bara na wa pwani,
Wazalendo kupendana, huo ndio uungwana.

**JITATHMINI**

1. Shairi hili lina beti ngapi?
2. Kulingana na shairi hili, unaona ‘mzalendo’ ni mtu wa aina gani?
3. Taja kibwagizo cha shairi hili.
4. Katika ubeti wa nne, ni mambo gani wazalendo wanafaa kufanya ili kusonga mbele?
5. Mtu anayetunga mashairi huitwa?
6. Taja vina vya kati vya ubeti wa pili.

## SI HOJA YETU JINSIA

**Mtunzi: Sophie Binsari**
**Lakabu: Tarabizuna ya Jangwani**
**Gatuzi : Kisii**

Hima hima twajongea, zetu sauti twapaza,
Ari metusisimua, letu wazo kuangaza,
Ukweli twawaletea, usawa tunatangaza,
Si hoja yetu jinsia, ubaguzi twa’kataza.

Sitazame linda lake, mawazo ukabadili,
Huyo mtoto wa kike, alivyo umkubali,
Siku zote asikike, haki zake muzijali,
Si hoja yetu jinsia, ubaguzi twa’kataza.

Sighairi yako nia, kwa kaptura ‘lovaa,
Sidinde wajibikia, haja kumtimizia,
Siwaze kumpuzia, wapaswa ‘mhudumia,
Si hoja yetu jinsia, ubaguzi twa’kataza.

Tupeni sote thamani, haki zetu ‘timizie,
Elimu tukabidhini, vitabuni tupitie,
Maarifa tupateni, wote tuwapasishie,
Si hoja yetu jinsia, ubaguzi twa’kataza.

## JITATHMINI

1.Shairi hili ni la aina gani? Eleza sababu

2.Kila ubeti wa shairi una mishororo mingapi?
3.Taja kibwagizo cha shairi hili.
4.Eleza ujumbe unaozungumziwa katika shairi hili.
5.Onyesha jinsi ubaguzi wa kijinsia unavyoendelezwa katika jamii yako.

**TUSHABIKIE MICHEZO**
**Mtunzi: Momanyi Henry**
**Lakabu: Ustadh Momanyi**
**Gatuzi**: **Trans- Nzoia**
Kandanda marufu soka, miguu hino hutumia,
Uwanjani hufurika, mashabiki kwa mamia,
Tushabikie michezo, kwa yetu  hali na mali.

Voliboli ya mikono, wachezaji 'kiwa sita,
Hupigwa kwayo mikono, kuuondoa utata,
Tushabikie michezo, kwa yetu hali na mali.
Pete ama netiboli, zenye goli mlingoti,
Milingoti ni miwili, yakupasa jizatiti,
Tushabikie michezo, kwa yetu hali na mali.

Hoki nayo yapendeza, na huchezwa kwa magongo,
Wachezaji 'napocheza, nao hupinda migongo,
Tushabikie michezo, kwa yetu hali na mali.

Kriketi hufarahisha, mchezo wa timu mbili,
Pia huwajumuisha, 'chezaji toka kuwili,
Tushabikie michezo, kwa yetu hali na mali.

Raga yahusisha nguvu, ikichezwa na waume,
Hutumia nyingi nguvu, hasa wana wa kiume,
Tushabikie michezo, kwa yetu hali na mali.

Karate ya kijapani, ya miguu na mikono,
Asili yake japani, ya kupangua mikono,
Tushabikie michezo, kwa yetu hali na mali.

Chesi huchezwa kwa bao, wahusika 'kiwa wawili,
Vipira juu ya mbao, husogezwa kwa akili,
Tushabikie michezo, kwa yetu hali na mali.

Mbio huwa anuwahi, hasa kule uwanjani,
Kasi iliyo sahihi, huchuja washindani,
Tushabikie michezo, kwa yetu hali na mali.

Msabaka una raha, ndio mbio za farasi,
Yatuletea furaha, tokana na yake kasi,
Tushabikie michezo, kwa yetu hali na mali.

**JITATHMINI**

1. Taja aina ya mchezo unaohusisha farasi
2. Toa msamiati mwingine kwa mujibu wa shairi unaomaanisha kandanda
3. Ni aina gani ya mchezo unanishirikisha wachezaji sita kulingana na shairi hilo?
4. Taja asili ya mchezo wa karate
5. Mchezo upi huchezwa kwa magongo?

**MAKAO YA VIUMBE**
**Mtunzi: Wambani Okwalo Henry**
**Lakabu: Malenga wa Mitume**
**Gatuzi**: **Busia.**

Sikiza mwanafunzi, jifunze msamiati,
iwe yako kurunzi, kutoa atiati,
makao ya viumbe, makao ya viumbe,
uyatie kichwani.

Zizini ni kwa ng'ombe, bandani kwa nguruwe,
Kizimba au kirimba, hapo mpate kuku,
Upwa, ni kwa mbwa, na chaani utapata farasi.

Mzingani kwa nyuki, masega ni kwa jana,
panzi naye nyasini, konokono kombeni,
Shimoni ni kwa panya, na pangoni nenda mpate nyoka.

Kiota au sasa, hapo mpate nyuni(ndege),
Utandabui jamani, mwenyeji buibui,
Kiwavi fukofuko, na kasuku mwenyeji wa tunduni.

Mfalme ni kasrini, rais ikuluni,
Wavulana shuleni, watalala ganeni,
Dahalia watalala, wasichana shuleni.

Dereva ni usukani, dunguni kwa rubani,
Kidurusi/kingulima/kichuguu, ni kwa mchwa,
Mfungwa gerezani,husunini au hata ngomeni.

Samaki naye majini, fuko kwake shimoni,
Wanajeshi kambini,kasisi kanisani,
Mchawi kilingeni, mtawala kwake ni kitalani.

JITAHMINI.

1. Ng'ombe huishi zizini kama vile ----- nyasini.
2. Makao ya wasichana shuleni ni?
3. Ukitaka kumfuga kuku, lazima uunde -------
4. ------- ndipo wanapikaa wachawi wanapofanya uchawi.
5. Makazi ya konokono ni?

**Mtunzi: Wambani Okwalo Henry**
**Lakabu: Malenga wa Mitume**
**Gatuzi**: **Busia.**

Mdomoni tuna hinalisa,
nayo ndonya haikosekani,
kidomwa ukipenda shedo,
utapamba mdomo.

Huku puani tunacho kipini,
Kishaufu, hazama, kikero,
Ukipenda hata na shemere,
Utapamba puani.

Sikioni tunayo herini,
Bali, kipuli au togo,
Nti, jasi hata jaribosi,
Ukipenda mapete.

Shingoni ukoja, mkufu,
Kidani, ushanga nayo timba,
Koja, kigwe, usinga, kikuba,
Useja, kinagiri.

Miguuni tunazo furungu,
Udodi, hina na milia,
Njuga, wanja, nyerere, kugesi,
Ukipenda, kikuku.

Macho yote twayarembesha,
Kwa miwani hata nayo wanja,
Hayo yote kweli ni mapambo,
Machoni twapamba.

Usoni tunayo chale,
Toja, gema, nembo na traruma,
barakoa hata nayo paku,
Utapamba usoni.

Nywele/ kichwa tunayo ngeu,
Pini,taji, hina, kibanio,
Ukipenda hata nayo shela,
Utapamba nywele/ kichwa.

Mkononi tunayo bangili,
Usinga, wanja, hina, pochi,
Nembo, pingo, udodi, kikuku,
Ukipenda kekee.

JITATHMINI

1. Taja pambo linalopamba mguu na mkono.
2. Ukitaka kupamba pua utapamba kwa mapambo gani?
3. Pambo linalopamba midomo huitwa ------ au -----
4. Nywele hubanwa kwa ----
5. Mkufu, ushanga na kikuba hupamba sehemu gani ya mwili?

**MSHIKAMANO WA TAIFA**
**Mtunzi: Momanyi Henry Rioba**
**Lakabu: Ustadh Momanyi**
**Gatuzi**: **Trans- Nzoia.**

Taifa lapaswa kuwa, na ushikamano mwema
Sote twahitaji kuwa, waja wenye nia njema
Mshikamano ni nguzo, kwa taifa kusitawi

Umoja kweli ni nguvu, utengano udhaifu
Twapaswa kuwa shupavu, bali tusiwe hafifu
Mshikamano ni nguzo, kwa taifa kusitawi

Ushikamano ni bora, kwayo nchi kusitawi
Nani apenda hasara?, Nauliza hata Malawi
Mshikamano ni nguzo, kwa taifa kusitawi

Nacho kidole kimoja, kweli hakivunji chawa
Tuuimbe wimbo moja, wa umoja na usawa
Mshikano ni nguzo, kwa taifa kusitawi

Daima Kinga na Kinga, ndio moto huwaka
Msingi imara jenga, ili tuje faidika
Mshikamano ni nguzo, kwa taifa kusitawi

Unafiki mbali weka, tupendane sisi site
Sote tutafaidika, pasi lawama yoyote

Mshikamano ni nguzo, kwa taifa kusitaw

**JITATHMINI**

1. Taja umuhimu mbili ya ushikamano kulingana na shairi hili
2. Toa methali mbili alizotumia mwandishi wa shairi hili
3. Taja neno lingine lenye maana sawa na 'lawama'
4. Andika kibwagizo cha shairi hili
5. Orodhesha madhara mawili ya taifa isiyozingatia mshikamano ukizingatia shairi hili

**TUUPINGE UGAIDI**
**Mtunzi: Agadias Ikoha**
**Lakabu: Malenga wa Nyali one**
**Gatuzi : Mombasa**

Shairi ninalighani, hadharani lisikike,
Popote 'mi nalighani, watu wote walishike,
Ugaidi duniani, ombi langu upingike,
Tuulenge ugaidi, tuishini kwa amani,

Dini tuwajibikeni, amani kuineza,
Mabaya tukashifuni, ugaidi umeoza ,
Mema tuyahubirini, vijana kuwahimiza,
Tuulenge ugaidi, tuishini kwa amani.

Sheria tuzibunini, zile za kutulindeni,
Kishikwa ugadini, hukumu mahakamani,
Jela iwe mpangoni, magaidi kifungoni,
Tuulenge ugaidi, tuishini kwa amani.

Wazazi huko nyumbani, wenu wana walindeni,
Mafunzo wana wapeni, maadili wafunzeni,
Siwaache mitaani, nawasihi wachungeni,
Tuulenge ugaidi, tuishini kwa amani.

Naiomba serikali, nafasi tengenezeni,
Za kazi muwakabidhi, vijana kote nchini,

Ugaidi tukabili, usikuwepo jamani,
Tuulenge ugaidi, tuishini kwa amani.

Wengi twataka nidhamu, ugaidi tuondoe,
Heshima kote idumu, ujambazi tuutoe,
Kwenu washika hatamu, kote watu muokoe,
Tuulenge ugaidi, tuushini kwa amani.

Ugaidi sio kitu, faida kweli hauna,
Ugaidi huna utu, ovyo mavuno huvuna,
Mateso kwetu 'si watu, twapata kwa kumizana,
Tuulenge ugaidi, tuishini kwa amani.

Una mambo ugaidi, mengi tena yakudhuru,
Unaleta uhasidi, watu wakosa uhuru,
Kuogopa yawabidi, wanaishi kwayo hofu,
Tuulenge ugaidi, tuishini kwa amani.

**JITATHMINI**

1)Kibwagizo katika kila ubeti kina mizani ngapi?
2)Ugaidi una athari zipi?
3)Eleza maana ya misamiati ifwatayo; Uhasidi, Maadili
4)Shairi hili ni la aina gani?
5)Wazazi wanahimizwa wafanye nini?

**WAHISANI MKO WAPI?**
**Mtunzi: Agadias Ikoha**
**Lakabu: Malenga wa Nyali one**
**Gatuzi : Mombasa**

Mwenzenu mimi jamani, kuna ninayowazia,
Yaniweka mawazoni, malenga nafikiria,
Wapo waja duniani, shida wanazipitia,
Wahisani mko wapi, mje muwasaidie.

Mje muwasaidie, wakapate afueni,
Msaada uwafae, wapate toka shindani,
Chochote muwapatie, kuwekeza jalieni,
Wahisani tokezeni, dunia kuiongoa.

Dunia kuiongoa, walemavu watulie,
Shida ziweze kupoa, zaliwa wasijutie,
Wezesheni kutoboa, maisha wafurahie,
Wahisani fadhilini, miradi zao zifane.

Fanyeni yalo ya kweli, mkafike vijijini,
Mfike kila mahali, sipendelee mijini,
Wabara muwafadhili, nao wawe furahani,
Kote kuwepo usawa, ubaguzi usiwepo.

Miradi zao zifane, waweze jitegemea,
Mwanga wao waone, kiza waweze kemea,

Kokote kule wanene, wapate kujitetea,
Wahisani wenye haja, fanyeni yalo ya kweli.

Fanyeni yalo ya kweli, mfike na mashuleni,
Wasomi muwabadili, karo  kuwalipieni,
Wajazwe wao akili, wafaulu maishani,
Wahifadhini wasomi, watimize zao ndoto.

**JITATHMINI**

1)Tarbia ni shairi lenye mishororo mingapi katika kila ubeti?
2)Shairi hili lina beti ngapi kwa jumla?
3)Mshororo wa mwisho katika kila ubeti umerudia tutauitaje ?
4)Shairi hili lina vipande vingapi?
5)Kipande cha kwanza katika ubeti wa pili mshororo wa kwanza cha semaje?

**AJIRA**
**Mtunzi: Alfred Lobawoi**
**Lakabu: Mweledi Chipukizi**
**Gatuzi : Turkana**

**Mwanafunzi**: Nimekuja leo kwako, kuomba usaidizi,
Nilikotokea huko, nilikuwa kijakazi,
Mimi ndiye punda huko, kufanyishwa yote kazi,
Mbona akaniajiri, na sijafikisha mwaka?

CHIFU: Sikupati mwana wangu, hebu sasa unieleze,
Najua una machungu, tafadhali nisikize,
Uketi karibu yangu, hayo yote unijuze,
Ni kinyume cha sheria, anafaa tu kifungo.

Mwanafunzi: Naishi na nyanya yangu, tangu zama za zamani,
Alipoaga Ninangu, kuondoka duniani,
Alifuata Babangu, kuniacha kilioni,
Mbona akaniajiri, na sijafikisha mwaka?

CHIFU: Ninakupata vizuri, hata nalia moyoni,
Maisha hayo shubiri, yananikata maini,
Sasa yapi yalijiri, kutoka hapo mwanzoni?
Ni kinyume cha sheria, anafaa tu kifungo.

Mwanafunzi: Nilijipata kazini, kwa tajiri mwenye mali,
Kazi zote za nyumbani, zikanifunga kufuli,

Sikwenda hata shuleni, nilipambana na hali,
Mbona akaniajiri, na sijafikisha mwaka?

CHIFU: Nyanya yako yuko wepi, mbona naye kakubali?
Anajua kosa lipi, litakalomkabili?
Atajua ni mangapi, ili tena asifeli,
Ni kinyume cha sheria, anafaa tu kifungo.

Mwanafunzi: Nyanya pia aliendа, kwa njia ya marahaba,
Nimebaki na kidonda, kisichokuwa na twiba,
Sikuwa na pa kuenda, ndo akaja huyu Baba,
Mbona akaniajiri, na sijafikisha mwaka?

CHIFU: Pole sana mwana wangu, kwa hayo yalokufika,
Maadamu upo kwangu, sasa nitashughulika,
Usiachie machungu, nena yote naandika,
Ni kinyume cha sheria, anafaa tu kifungo.

Mwanafunzi: Baba huyu ni mkwasi, ambaye ananitesa,
Ananifanya unyasi, kukanyanga bila kosa,
Kila siku wasiwasi, nitaenda wapi sasa?
Mbona akaniajiri, na sijafikisha mwaka?

CHIFU: Hasa ni mateso gani, ambayo anayatenda,
Hali hii ya huzuni, ni vipi yeye mtenda?
Hanayo utu kwa nini, kwa hayo anayotenda?
Ni kinyume cha sheria, anafaa tu kifungo.

Mwanafunzi: Kazi zote za sulubu, na sili hata chakula,
Sipewi hata kitabu, na pahala pa kulala,
Nimesalia kibubu, nalala hata kwa ghala,
Mbona akaniajiri, na sijafikisha mwaka?

CHIFU: Ni vizuri umesema, hayo yote yametosha,
Serikali imesema, maisha inaboresha,
Hali hii ya hujuma, leo hii imekwisha,
Ni kinyume cha sheria, anafaa tu kifungo.

CHIFU: Nitamtia nguvuni, akahukumu kifungo,
Ataishi gerezani, kwa huo mmoja mwongo,
Asidhani ni utani, hatutaki hata hongo,
Ni kinyume cha sheria, anafaa tu kifungo.

**KUJITATHMINI**:
1. Lipe shairi hili kichwa mwafaka.
2. Shairi hili linaitwaje?
3. Msimulizi wa shairi hili hana Baba na mama kwa hivyo ina maana kuwa yeye ni?
4. Taja malalamishi anayota mwanafunzi kuhusu mwajiri wake.
5. Mwongo mmoja ni kipindi cha miaka mingapi?
6. Eleza maana ya "Njia ya marahaba?"
7. Taja neno lingine lenye maana sawa

**LISHE BORA**
**Mtunzi: Michael Cosmas**
**Lakabu: Malenga wa Sayari Kavu**
**Gatuzi : Kitui**

Karibu karibu nyote, tule vyakula vitamu,
Yako sahani ulete, tule viazi vitamu,
Nguvu nyingi na tupate, tulapo viazi vitamu,
Kaka dada usisite, daktari na mwalimu,
Afya njema na tupate, kwa lishe bora na tamu,
Tule lishe bora sote, kiafya tuwe imara.

Mahindi pia tuleni, ya kuchoma na chemsha,
Uji mtama tunyweni, nguvu yetu sije isha,
Matunda mengi sokoni, tule pasi kubisha,
Tule matunda jamani, magonjwa sije kabisha,
Pia tupande shuleni, matunda yasije isha,
Tule lishe bora sote, kiafya tuwe imara.

Kuna matunda tofauti, kama machungwa tufaha,
Maembe ni tofauti, kubwa ndogo yenye raha,
Tule pasi masharti, tusije pata karaha,
Pasua papai kati, tule sote kwa furaha,
Tusiwe na hatihati, tukila kifasaha,
Tule lishe bora sote, kiafya tuwe imara.

Tule vingine vyakula, vyakula kama asali,

Ugali tamu chakula, hasa mchicha ugali,
Ukunywe maziwa lala, maziwa glasi mbili,
Pia baada ya kula, ni maji glasi mbili,
Tule vya afya vyakula, unawiri wetu mwili,
Tule lishe bora sote, kiafya tuwe imara.

Kuna pia vya asili, kama mihogo na duma,
Viungo vya pilipili, tutie ndani ya nyama,
Vyakula vya kiasili, tusiviache nyuma,
Na mboga za kiasili, terere tule kwa sima,
Vyakula vya uswahili, pweza na tumle nyama,
Tule lishe bora sote, kiafya tuwe imara.

Kuna vyakula fulani, mwilini vina madhara,
Sukari nyingi mwilini, na soda vina madhara,
Keki chipsi mwilini, peremende ni hasara,
Chumvi nyingi mwilini, kunayo mengi madhara,
Chokoleti epukeni, hakika si masihara,
Tule lishe bora sote, kiafya tuwe imara.

Kikomo sasa natia, nacheni nende nyumbani,
Yangu hayo zingatia, ya lishe bora jamani,
Lishe bora fuatia, mchana pia jioni,
Asubuhi ni hatia, kutotia mdomoni,
Akilini nomba tia, zingatie maishani,
Tule lishe bora sote, kiafya tuwe imara.

**KUJITATHMINI**

1. Taja vyakula vinavyoweza kuleta afya nzuri.
2. Taja viungo vinavyotumika kupikia chakula
3. Taja vyakula vya asili vilivyotajwa.
4. Mwili utakuwa na afya ikiwa utakula vyakula gani?
5. Shairi hili lina beti ngapi?

**NZI KUFA KIDONDANI**
**Watunzi: Momanyi Henry na Elisha Otoyi**
**Lakabu: Ustadh Momanyi na Malenga wa Wanyonge**
**Magatuzi : Trans Nzoia & Homabay**

**Elisha otoyi**
Dhilali nilopitia, zimenizidi yakini,
Kijaribu nyamazia, huzuni menisheheni,
Dinasi nimalizia, maishangu duniani,
Hakuna alobobeka, kichango kuchangizana.

**Momanyi**
Wapenda kulalamika, tatizo mie sioni,
Ati wazidi kumaka, nakutia mashakani!
Maji mekwisha mwagika, mimi na wewe mbioni,
Hakunaa alobobeka, kichango kuchangizana.

**Elisha otoyi**
Ndugu nakubembeleza,si kuwa ni hatarini,
Hatima yako nawaza,takavyoishi mbeleni,
Sione mekukataza,najali mwako 'ushini,
Hakuna alobobeka, kichango kuchangizana.

**Momanyi**
Mashine mejitwalia, miti hii taabani,
Aghalabu nawazia, nijitome msituni,
Muda unavyokimbia, niuage umaskini,

Hakunaa alobobeka, kichango kuchangizana.

**Elisha otoyi**
Wakumbuka zile pesa,ukapata utalini?
Nabashiri utakosa, kuzipata mfukoni,
Ndo maana yakupasa, kunikuza kwa makini,
Hakuna alobobeka, kichango kuchangizana.

**Momanyi**
Kukwambia sina budi, darahimu mifukoni,
Tena mbao nafaidi, yaenda ughaibuni,
Nafanya kwa makusudi, nikifyonza ja kunguni,
Hakuna alobobeka, kichango kuchangizana.

**Elisha otoyi**
Miti yangu meikata, mingine kufanya kuni,
Jangwa nalo ukaita, piga kambi kijijini,
Faida utazopata, uliza zipi lakini?
Hakuna alobobeka, kichango kuchangizana.

**Momanyi**
Nayo nachoma, sijue ngapi matani,
Na hili halitakoma, hakika sio utani,
Kiholela ninachoma, wakunizuia nani?
Hakuna alobobeka, kichango kuchangizana.

**Elisha otoyi**

Nakuambia kiburi, takutia mashakani,
Tarajia zako shari, umekuwa na shetani,
Nakuonya jihadhari, yako yapo ukingoni,
Hakuna alobobeka, kichango kuchangizana.

**Momanyi**
Natenda ninavyopenda, amadi i kibindoni,
Nilokata sijapanda, 'tamea kama zamani,
Haja gani kuyapanda, ilhali yupo manani?
Hakunaa alobobeka, kichango kuchangizana.

**Elisha otoyi**
Usingizi mekosesha, hata wetu hayawani,
Makazi yao meisha, kwa pupa zako za peni,
Wengine umewafisha, komango masikioni,
Hakunaa alobobeka, kichango kuchangizana.

**Momanyi**
Bado menijaa mie, tamaa hadi pomoni,
Ninahisi nisalie, kikutia hatarini,
Uje hata ujutie, ulipo pale shimoni,
Hakunaa alobobeka, kichango kuchangizana.

**Elisha otoyi**
Umewahi jiuliza, maisha si ja zamani?
Mbona ziwa lajikaza, kupaacha ufuoni,
lokubakia ni kiza, To! To! Ro! funika mboni,

Hakunaa alobobeka, kichango kuchangizana.

**Momanyi**
Maji chafu 'fungulia, kuelekea ziwani,
Viwanda vyaachilia, moshi kufuka angani,
Mtimani 'furahia, vioja 'livyosheheni,
Hakuna alobobeka, kichango kuchangizana.

**Elisha otoyi**
Ukiomba unapewa, 'twike sasa mgongoni,
Lawama ulowekewa, tamiliki aushuni,
Sitotaka kuambiwa, shida zako abadani!
Hakuna alobobeka, kichango kuchangizana.

**Momanyi**
Kwa hakika limewaka, lachoma hadi wayoni,
Ziwani 'meadimika, viumbee vya majini,
Misitu 'memalizika, nilipo ni taabani,
Hakuna alobobeka, kichango kuchangizana.

**Elisha otoyi**
Rohoni nasikitika, nilivyoo hayawani,
Machungu yamenifika, 'menisakama kooni,
Maisha 'mebadilika, 'merejea umaskini,
Hakuna alobobeka, kichango kuchangizana.

**Momanyi**
Ni jambo lilo busara, kaniki toa matoni,
Nakupa zangu hongera, kwa kauliyo 'timani,
Kwaheri sasa 'fukara, bai hadi hawindeni,
Hakuna alobobeka, kichango kuchangizana.

**JITATHMINI**

1.Lipe anwani mwafaka shairi hili(alama 2)

b.Katika ubeti wa sita taja aina ya vyakula vinavyoweza kuleta uharibifu mwilini kama alivyoelezea mtunzi wa shairi hili(alama 4)

2.Shairi hili ni la bahari gani?Toa sababu (alama 4)

3.Huku ukitolea mifano mwafaka,taja arudhi zinazotumika katika ubeti wa tatu(alama 4)

4.Andika ubeti wa pili kwa lugha nathari(alama

5.Eleza maana ya maneno yafuatayo(alama 3) Karaha, Nawiri, Madhara

**TUJIFUNZE TASHBIHI**
**Mtunzi**: **Bright Odeng**
**Lakabu** : **Nuru gizani.**
**Gatuzi**: **Siaya**

Simba ndiye mfalme porini,manyoya rangi majani makavu
Mnyama mkali sana,alaye nyama
Jamii yake paka,tunasema mkali kama simba

Fisi sifa yake ulafi,rangi yake kijivu
Ukubwa wake ni wa beberu,mnyama mwoga sana
Alaye mizoga,tunasema mlafi kama fisi

Twiga ana shingo ndefu,mwenye mabatobato meusi
Hupatikana barani Afrika,hula majani ya miti
mnyama mrefu sana,tunasema mrefu kama twiga

Sungura aishiye porini,mdogo sana masikio yake marefu,
Tunamjua kwa ujanja wake,tunasema mjanja kama sungura

Swara pia huitwa swala,hufanana na mbuzi mkubwa
Kuna aina nyingi ya swara,mnyama wa porini
Anasifika kwa mbio ya kasi,mbio ya kasi kama swara

Tunafika kwa kobe ana gamba gumu sana
Shingo yake fupi,anaishi porini na kwa maji
Aendaye polepole,mwendo pole kama kobe

Nguruwe hufugwa nyumbani,pia huitwa hinziri
Ana pua kubwa na ndefu,mguu na mkia mfupi
Aliye mfupi na mnene,tunasema mnene kama nguruwe

Tausi huwa na madoadoa,yenye rangi nyingi
Duma huwa na mkia mpana,rangi ya buluu na kadhalika
Ni aina ya ndege,mwenye maringo kama tausi

**JITATHMINI**

1.Mamangu ni mkali kama___________________

2.Mtoto yule ni mlafi kama___________________

3.Tunasema mrefu kama____________________

4.Tunasema mnene kama___________________

5.Mgonjwa anatembea polepole kama_______

**MAVAZI YETU**
**Mtunzi**: **Bright Odeng**
**Lakabu** : **Nuru gizani.**
**Gatuzi**: **Siaya**

Aina nyingj mavazi, huvaliwa mwilini
Ya kwanza ni chupi, nguo ndogo sana
Huvaliwa kiunoni, kufunika sehemu ya siri

Ya pili sidiria, wanawake huivaa
Ina vifuko viwili, vishikavyo matiti
Pia huitwa kanchiri

Shimizi vazi jingine, vazi jepesi sana
Huvaliwa na wanawake, mle ndani ya rinda
majina yake mengine, ni shumizi nakamisi

Chepeo huvaliwa kichwani, ukingo wake nusu duara
Ukingo wake hujitokeza mbele, kutukinga kwa jua kali
Jinsia yote huivaa, waume huipenda zaidi

Skafu huvaliwa shingini, na pia mabegani
Hutukinga kwa baridi, kutofika mwilini
Pia huweza kuwa mtandio, na kufungwa kwa kichwa

Soksi huvaliwa mguuni, kablaya kiatu kuvaliwa
Hutukinga baridi, kutoka kwa miguu yetu

soksi ni vazi ndogo, na huvaliwa na jinsia yote

Tai ni kama kitambaa, huvaliwa shingoni
Hufungwa ukosini mwa shati, na pia mwa blauzi
Kisha kufungwa fundo tu, mbele ya shingo

**JITATHMINI**

1. Vazi lipi huvaliwa kiunoni kutufunika uchi
2. Taja kisawe cha shimizi.
3. Vazi livaliwalo wanawake kusetiri maziwa huitwa?
4. Soksi huvaliwa na jinsia gani?
5. Ukosi ni nini?

**NAKUPENDA USHAIRI**

**Mtunzi: Timothy Omusikoyo Sumba**

**Lakabu: Malenga Mstaarabu**

**Gatuzi : Kakamega**

Naupenda ushairi, ni fani ilotukuka,
Ikipangwa mistari, moyo huniburudika,
Vina  mukivikariri,machofu huniondoka,
Ushairi fani tamu, nanaipenda hakika.

Unayasema ya siri, huku watu wanacheka,
Maovu wayahubiri, kwa lugha ilotukuka,
Wayatoa ya kaburi, bila kuzinga mashaka,
Ushairi fani tamu, nanaipenda hakika.

Lughaye huwa nzuri, vyema ilio katika,
Ilopangika vizuri, kwa taratibu mwafaka,
Hainavye machachari, ni fani ino sifika,
Ushairi fani tamu, nanaipenda hakika.

Mtunzi huyakithiri, ambayo anayataka,
Akapasua bahari, vidagaa kuvishika,
Akamtoa jodari, lengo likatambulika,
Ushairi fani tamu, nanaipenda hakika.

Ushairi kama nari, vibaya vinachomeka,
Mtunzi hawi na shari, lengo ujumbe kufika,
Ukaenea viriri, Mombasa na hadi Makka,
Ushairi fani tamu, nanaipenda hakika.

Ushairi ni shubiri, maradhi yanaondoka,
Ushairi daktari, tiba zimeshatufika,
Umesafisha dahari, zote zikanawirika,
Ushairi fani tamu, nanaipenda hakika.

Ushairi ni johari, umati waaelimika,
Ukayavunja magari, baskeli zikashika,
Ushairi ninakiri, ladhaye inasifika,
Ushairi fani tamu, nanaipenda hakika.

**JITATHMINI**

1. Je, shairi hili ni la aina gani?
2. Je, shairi hili lina beti ngapi?
3. Eleza ujumbe muhimu katika shairi hili.
4. Andika vina vya mwisho katika shairi hili
5. Andika mshororo wa tatu katika ubeti wa tatu.

**TUYAPENDE MAZINGIRA**
**Mtunzi: Wilberforce Keya**
**Lakabu: Malenga wa Musanda**
**Gatuzi : Kakamega**

Apendaye mazingira, ovyo hatatupa taka,
Apendaye mazingira, hachanjichanji kwa shoka,
Apendaye mazingira, maenge atayateka,
Tuyatunze mazingira, mazingira yatutunze.

Apendaye mazingira, lazima atarembesha,
Apendaye mazingira, kutunza hakutachosha,
Apendaye mazingira, moto chaka hatawasha,
Tuyatunze mazingira, mazingira yatutunze.

Apendaye mazingira, ovyo hatakata miti,
Apendaye mazingira, kutunza hujizatiti,
Apendaye mazingira, faidaye si katiti,
Tuyatunze mazingira, mazingira yatutunze.

Apendaye mazingira, miti itashiba maji,
Apendaye mazingira, hatayakosa malaji,
Apendaye mazingira, ndiye avikwaye taji,
Tuyatunze mazingira, mazingira yatutunze.

Apendaye mazingira, hataua hayawani,
Apendaye mazingira, huhifadhi vya nyikani,

Apendaye mazingira, amtukuza Manani,
Tuyatunze mazingira, mazingira yatutunze.

Apendaye mazingira, atahamasisha waja,
Apendaye mazingira, manufaa ataja,
Apendaye mazingira, atapata lake koja,
Tuyatunze mazingira ,mazingira yatutunze.

**JITATHMINI**

1. Taja mbinu za kutunza mazingira.
2. Anayependa mazingira hafanyi nini?
3. Taja njia za kutunza miti.
4. Shari hili ni la aina gani?
5. Mazingira yakiwa machafu tunaweza kupata nini?

**HISABATI**
**Mtunzi: Wilberforce Keya**
**Lakabu: Malenga wa Musanda**
**Gatuzi : Kakamega**

Kipeo natanguliza, zidisha hiyo nambari,
Hapa pia nakujuza, siihusishe sufuri,
Nambari kutotatiza, ni kujua yake siri,
Hisabati sio ngumu, fanya KIMAGAZIJUTO.

Mabano kwenye hesabu, yasikutie kiwewe,
Utalipata jawabu, swali hilo lielewe,
Yani je sikupe tabu, ya ndani izidishiwe,
Hisabati sio ngumu, fanya KIMAGAZIJUTO.

Gawanya hizo idadi, pa swali ulotengewa,
Zigawe ukiradidi, gawa ulivyoambiawa,
Tafakari nyuma rudi, usahihi kuridhiwa,
Hisabati sio ngumu, fanya KIMAGAZIJUTO.

Zidisha ndiko kukuza, idadi kuongezeka,
Wala sio kupunguza, ni sawa na kutanuka,
Mbili na mbili wawaza, nne umeshaishika,
Hisabati sio ngumu, fanya KIMAGAZIJUTO.

Jumlisha ufahamu, idadi weka pamoja,
Ndio msingi elimu, mwalimu atautaja,

Elewa na ufahamu, mbili ni moja na moja,
Hisabati sio ngumu, fanya KIMAGAZIJUTO.

Toa zikihesabika, idadi uloulizwa,
Fahamu zitapunguka, kinyume cha kuongezwa,
Na kando utaziweka, zile zilizopunguzwa,
Hisabati sio ngumu, fanya KIMAGAZIJUTO.

**JITATHMINI**

1. Eleza maana ya neno kiwewe ukirejelea kamusi yako.
2. Taja ishara za hisabati zilizotajwa ushairini
3. Taja methali inayoendana na kibwagizo cha shairi hili
4. Shairi hili Lina mizani mingapi?

**METHALI ZA KISWAHILI**

**Mtunzi: Masika Derrick**

**Lakabu : Dokta Ziro**

**Gatuzi: Kakamega.**

Ewe mwanangu sikia, maisha yana mipango,
Hivi leo nakuambia, nabisha wako mlango,
Nakupa wangu wosia, huo ni wangu mchango,
Mali bila daftari, hupotea bila habari.

Shika mambo yake mama, usije ukapotea,
Ukaja kushika tama, mabaya yakitokea,
Kidete wewe simama, utakuja kupepea,
Asiyefunzwa na mama, hufunzwa na ulimwengu.

Sikio lako fungua, usije kutia pamba,
Nawe ukajiumbua, kwa sifa ukajigamba,
Moyo wako kama ua, tena safi kama pamba,
Sikio lile la kufa, na halisikii dawa.

Subira weka moyoni, subira huvuta heri,
Japo tabu maishani, dhiki nyingi kwa safari,
Usife matumaini, mbeleni takuwa heri,
Kila mwenye kusubiri, mwisho budi ale mbivu.

Mlaani afiriti, asijekuteka nyara,

Msimamo weka tisti, dhabiti tena Imara,
Panga yako mikakati, uondokeweadhara,
Bura yako sibadili, kwa faida ya rehani.

Shairi langu kiasi, tamati hapa nafika,
Naye Mungu simuasi, ukaja kutaabika,
Kwake kunayo nafasi, ewe mwanagu pulika,
Naye Mungu hamuachi, yule alo mja wake.

**Jitathmini**

1. Shairi hili ni la aina gani ?
2. Ubeti wa kwanza una mishororo mingapi ?
3. Taja methali nyingine sawa na kibwagizo cha ubeti wa tatu .
4 . Ni nini maana ya neno **kutia** katika mshororo wa kwanza, ubeti wa tatu?
5 . Ubeti wa mwisho una mizani mingapi ?

**ADABU NI AKIBA**
**Mtunzi: Wafula P Wanjala**
**Lakabu : Mvua ya njaa**
**Gatuzi: Kakamega.**

Watoto watieeni, fuata zao amri,
Mkasikie maoni, mkikubali kwa ari,
Wavyele wenye amani, mkiishi bila kiburi,
Shikeni hii adabu, iwe akiba ya kesho.

Kiburi ndicho kaburi, ufunzwe na ulimwengu,
Usione ni hodari, kiburi kiwe ni pingu,
Utaenda kwa tanuri, ni adhabu yake Mungu,
Shikeni hii adabu, iwe akiba ya kesho.

Kataa ya ibilisi, fuata ya Mkawini,
Usipende ni fulusi, ikutie hatarini,
Ukijiona filisi, uibe pesa nyumbani,
Shikeni hii adabu, iwe akiba ya kesho.

Ukiitwa waitika, kwa sauti ya heshima,
Upate tele baraka, kutoka kwa abu, mama,
Heshimu dada kaka, bila tena kulalama,
Shikeni hii adabu, iwe akiba ya kesho.

**Jitathmini**

1. Taja vina vya ubeti wa tatu.
2. Mtoto akiwa na kiburi anastahili kufunzwa na nani?
3. Taja umuhimu wa kuwa na adabu na heshima.
4. Taja idadi ya mizani katika ubeti wa mwisho.
5. Taja kisawe cha fulusi.

**NATAMANI NENO**
**Mtunzi: Wafula P Wanjala**
**Lakabu : Mvua ya njaa**
**Gatuzi: Kakamega.**

Baba uliye mbinguni, nanena ni shukrani,
Natoa buka moyoni, naita tamu imani,
Nioshe mwangu moyoni, neno liwe akilini,
Injili ninatamani, nihubiri duniani.

Ninakataa machezo, neno ninalitamani,
Utadhani ni mchezo, ukweli uko moyoni,
Wale wapendao bezo, kona zote wafitini,
Injili ninatamani, nihubiri duniani.

Dunia hii ya tatu, kimepotoka kizazi,
Isi walo na mafutu, watoawo uamuzi,
Ukweli mtu ni watu, nisikie laazizi,
Injili ninatamani, nihubiri duniani.

Hawaendi ibadani, makao yao puyani,
Bia zao barazani, wakitoa ni maoni,
Uongo wa tumaini, jiona sudi jamani,
Injili ninatamani, nihubiri duniani.

Napiga yangu king'ora, hii tamu tena honi,

Kamsa ilo harara, ukatoke hatarini,
Hakuna tena abra, utahama duniani,
Injili ninatamani, nihubiri duniani.

Ndege yangu inatua, ikotoka ni angani,
Amenituma Jalia, turudini ibadani,
Hatimani tukalia, 'kupata siri sirini,
Injili ninatamani, nihubiri duniani.

**Jitathmini**

1. Shairi hili Lina beti ngapi?
2. Taja mazingira ya maudhui haya.
3. Eleza maana ya neno bezo.
4. Mwandishi ana tamani nini?
5. Taja majina ya Mungu

**NIMERUDI TENA**
**Mtunzi: Wafula P Wanjala**
**Lakabu : Mvua ya njaa**
**Gatuzi: Kakamega.**

Ninatoka huku hara, karibu na buldani,
Ninasimama imara, kunena ya siasani,
Ukabila wao sera, wazururuka nchini,
Huu moto wanawasha, ni nani atauzima?

Moyoni ninayo guma, na sio tena gumio,
Hadi sasa ninahema, kwa rabsha hizi zao,
Kila siku nikikema, kwa baya yao mazao,
Huu moto wanawasha, ni nani atauzima?

Wakijiona aali, maneno wabubujika,
Ili wawe bulibuli, kumbe wapenda vibaka,
Hali ikawe si hali, maovu wakitamka,
Huu moto wanawasha, ni nani atauzima?

Wamerudi viongozi, moyoni wametulia,
Wakitafuta ni kazi, mbinu zote kutumia,
Wakisema wazi wazi, amani watutakia,
Huu moto wanawasha, ni nani atauzima?

Beti tano ninatua, nakejeli wanafiki,

Wao wanajitakia, vyeoni ili wabaki,
Hatima itafikia, wakitungwa kwa mikuki,
Huu moto wanawasha, ni nani atauzima?

**Jitathmini**

1. Moto gani unaowashwa kulingana na shairi hili?
2. Ukabila unaeza kurudisha uchumu nyuma, andika insha ukielezea kauli hii.
3. Shairi la beti tano laitwaje?
4. Taja vina vya kati na vya mwisho katika ubeti wa nne.
5. Mwadishi anakejeli watu gani?

**TULINDE MAZINGIRA**
**Mtunzi: Erick Omondi**
**Lakabu: Babu Mesh**
**Gatuzi: Siaya**

Tuchukue tahadhari, ndiposa tuwe salama,
Tujue zile hatari, ili tusije kuzama,
Tupende yetu mandhari, kuyachafua kukoma.

Kila mara tufagie, tukiondoa uchafu,
Usafi tuzingatie, magonjwa yasiwe hofu,
Mwanga tuukaribie, usiwe mwanga hafifu.

Taka zitupwe kwa pipa, tuyalinde mazingira,
Tuvikusanye vichupa, visitulete madhara,
Uchafu tukiutupa, utatupea hasara.

Nyasi ndefu tuzifyeke, tuzuie malaria,
Vidimbwi tuvifunike, maji 'sikusanyikia,
Plastiki tusizike, kwani hazitaozea.

Miti mingi tuipande, itusafishie hewa,
Tusafishe kila pande, tukiacha kulemewa,
Mazingira tuyapende, ni baraka tulipewa.

**Jitathmini**

1. Shairi hili ni la aina gani? Toa sababu.

2. Taja sehemu za kutupa uchafu kulingana na shairi.
3. Mbona tunawe mkono kwa maji na sabuni tunapotoka msalani?
4. Eleza maeneo manne ya kudumisha usafi kulingana na shairi.
5. Taja kibwagizo cha shairi hili.

**USAWA WA KIJINSIA**
**Mtunzi: Georgina Nyatich**
**Lakabu: Bi. Makini**
**Gatuzi: Nyamira, Kenya.**

Maina : Furahi dada furahi, kuwa gugu limeng'olewa
Dada donda meliwahi, sote tumekombolewa,
Elimu sawa kuwahi, haki zetu kupokewa,
Tuunganeni mikono, tukuze vipawa vyetu.

Amina: Jana vaa njuga vyema, haki msingi pakata,
Lishe na makazi chuma, wazazi wetu mepata,
Afya zetu zi imara, kupiga maradhi vita,
Tuunganeni mikono, tukuze vipawa vyetu.

Maina: Tazama dada tazama, masomoni tumewika,
Hesabu sayansi daima, tumechagua kuwaka,
Hakuna kushika tama, wala nayeghafilika,
Tuunganeni mikono, tukuze vipawa vyetu.

Amina: Uwanja wa taaluma, mekumbatia sawia,
Udaktari tu daima, kama pacha twakalia,
Matinga tinga sukuma, inua uchumi njiani,
Tuungane mikono, tukuze vipawa vyetu.

Maina: Tabasamu dada tabasamu, meng'ara uongozini,

Nafasi twaa kwa zamu, thuluthi tatu bungeni,
Weledi chunga humu, jitolee kisabuni,
Tuungane mikono, tukuze vipawa vyetu.

Amina: Juu mikono inua, tumeingia kanisani,
Nena njili vumilia, katambe uongozini,
Nguvu ya sala minia, kuwalea duniani,
Tuungane mikono, tukuze vipawa vyetu.

Maina; Michezo bila aibu, kule mbele kusalia,
Letea Kenya dhahabu, pale mbali kumbatia,
Mtu sikufanye bubu, dada hakiyo katalia,
Tuunganeni mikono, tukuze vipawa vyetu.

Amina: Hakika kaka memena, mwanamke ametamba,
Jikoni si pake tena, yeye mwanamke pomba,
Hakizo atetea sana, bila wasiwasi mamba,
Tuunganeni mikono, tukuze vipawa vyetu.

Maina: Tazama dada tazama, wakati wenu mefika,
Sihofu kurudi nyuma, pamoja bila wahaka,
Umoja wenu daima, tapata mema hakika,
Tuungane mikono, tukuze vipawa vyetu.

Amina: Nashukuru sana kaka, umbali huu kufika,
Hatua kubwa mevuka, huru wetu imarika,
Taji kweli metuvika, sote pia twainyaka,

Tuungane mikono, tukuze vipawa vyetu.

**Jitathmini**

1. Hili ni shairi la aina gani? Toa sababu.
2. Taja maeneo sita ambapo mwanamke ametamba.
3. Hapo zamani mwanamke angesalia wapi?
4. Kwa nini mwanamke wa sasa ni pomba?
5. Taja kibwagizo cha shairi hili.

**LINDENI VYOO**
**Mtunzi: Alex Simiyu**
**Lakabu: Ustadh Kiamboni**
**Gatuzi: Transnzoia**

Usafi vyoo rakadha, mejaa tele mawele,
Tuwazie mambo kadha, kwa tajiri na mtule,
Nadhifu iwe rafadha, maisha mazuri kilele,
Hakika vyoo muhimu, tuzingatie usafi.

Ukosefu majumbani, lazagaa hili sumu,
Majini na ardhini, nyingi mauti takwimu,
Makazini viwandani, kipaumbele muhimu,
Hakika vyoo muhimu, tuzingatie usafi.

Ombi nyote wasikifu, Kenya nzima nawasihi,
Matokeo tahafifu, tutashukuru Illahi,
Chenu choo furahifu, sijasema kwa ,
Hakika vyoo muhimu, tuzingatie usafi.

Wakuu wajibikia, nchini wastarehe,
Kwa magonjwa tazamia, vijijini wafikihe,
Wazazi nanyi sikia, vyoo vingi tujengehe,
Hakika vyoo muhimu, tuzingatie usafi.

**Jitathmini**

1. Taja visawe vya ugonjwa.
2. Tumia kamusi yako kueleza maana ya maneno haya.
3. Shairi hili Lina beti ngapi?
4. Kwa nini tunafaa tuzingatie usafi wa vyoo.
5. Kibwagizo hiki kina mizani mingapi?

**TUKATAE NYANYASO**
**Mtunzi: Alex Simiyu**
**Lakabu: Ustadh Kiamboni**
**Gatuzi: Transnzoia**

Vilio vimezidia, unyanyasaji barani,
Yumkini yaelea, kama meli baharini,
Wakuu wamechelea, kudai yetu amani,
Hakika vita shubiri, yawasha bila huruma.

Wanafunzi wamegoma, kupata yao elimu,
Wanaona ni hatima, masomoni kuhitimu,
Yao mikono kwa tama,majonzi kuwahujumu,
Hakika vita shubiri, yawasha bila huruma.

Yanasa wafanyakazi, kupoteza mshahara,
Wenye domo watetezi, wamegeuka tambara,
Wengineo wateuzi, ni wajanja ja sungura,
Hakika vita shubiri, yawasha bila huruma.

Kwako Rabi alumina, twakuomba ukombozi,
Si wazee si vijana, wamekuwa wakimbizi,
Majukumu yao wana, meyatoroka wazazi,
Hakika vita shubiri, yawasha bila huruma.

**Jitathmini**.

1. Taja maudhui yanayojitokeza kwenye shairi hili.

2. Hili ni shairi la aina gani?
3. Kuna mizano mingapi katika shairi hili?
4. Vita vinaweza kuleta nini?
5. Eleza maana ya '*hakika vita shubiri*'

**HATUTAKI SIASA MBI**
**Mtunzi: Opetuh O. Philip**
**Lakabu: Malenga Mstahiki**
**Gatuzi: Nairobi**

Kila pambazuko hapa, ni cheche na malumbano
Wosia wangu nawapa, Epukeni mivutano
Amani idumu hapa, tusiwe na farakano
Siasa mbi hatutaki, si wazalendo halali
Tusikinai amani, tuishipo kwa pamoja
Kila mkenya thamani, basi idumu faraja
Vigogo sikilizeni, punguzeni zenu haja
Siasa mbi hatutaki, si wazalendo halali

Nia yenu twaimanya, kutugonganisha sisi
Vihela vyenu vyafanya, tuzushe kadamnasi
Twaridhia kufanya, amani sisi kwa sisi
Siasa mbi hatutaki, si wazalendo halali

Siasa bora twataka, hino nchi iboreke
Vyuo vingi kujengeka, masomo yaimarike
Barabara kuboreka, kwa wepesi zipitike
Siasa mbi hatutaki, si wazalendo halali

Tamatini 'mefika, wosia nimefikisha
Asilani sina shaka, ujumbe 'mewasilisha

Tumaini langu hakika, uzalendo 'tazidisha
Siasa mbi hatutaki, si wazalendo halali

**Jitathmini**.

1. Shairi hili ni la aina gani ?
2. Taja kibwagizo cha shairi hili ?
3.)Taja vina vya kati na vya mwisho katika ubeti wa pili ?
4. Shairi hili lina jumla ya beti ngapi ?
5. Ujumbe gani wajitokeza katika ubeti wa nne ?

**NIDHAMU KILA TULAPO**

**Mtunzi: Opetuh O. Philip**
**Lakabu: Malenga Mstahiki**
**Gatuzi: Nairobi**

Nisikilize mwanangu, nikueleze yalo muhimu
Nidhamu hapa pangu, ni bora tulapo humu
Wajali ndugu mwanangu, wabakishie vitamu
Nidhamu kila tulapo, naomba uzingatie

Kuketi na kutulia, ni lazima huku kwetu
Si vyema jipakulia, tuwajali wenzetu
Yote nakusimulia, dumisha adabu kikwetu
Nidhamu kila tulapo, naomba uzingatie

Si bora kula haraka, mlo kiasi kinywani
Kuramba vidole hakika, si sawa nakuelezeni
Hata mlapo bazoka, nidhamu idumu mezani

Kuomba vitu muhimu, vilivyo mbali upate
Kuzungumza kwa simu, si bora ebu ukate
Kunawa kila msimu, mikono usipakate
Nidhamu kila tulapo, naomba uzingatie

Tamati nimefika, nasaha nimefikisha

Sina mashaka hakika, ujumbe nimekupasha
Siha sheshe na baraka, Mola 'takunawirisha
Nidhamu kila tulapo, naomba uzingatie..

Jitathmini.

1.Kuna mizani ngapi katika ubeti wa kwanza?

2. Shairi hili linazungumzia umuhimu wa nini?

3. Shairi hili ni la aina gani?

4 .Anayetunga mashairi huitwaje?

5.Taja kibwagizo cha shairi hili ?

6.Shirikiana na wenzako katika vikundi, kutunga shairi kama hili, ubeti mmoja

**JIPE MOYO**
**Mtunzi: Kelvin Njoroge**
**Lakabu: Ustadh Muturi**
**Gatuzi: Transnzoia**

Waweza kuwa u tiki,maisha kwako uchovu
Wachekwa na halaiki,waonewa hata wivu
Maisha chungu ja siki,chozi kwako rovurovu
Kuwa na uvumilivu,Jalali ‘takujaliya

Mepoteza tumaini, imekunyanyasa tabu
Mekukimbia wandani, mejawa nyingi aibu
Nanga kwako mtimani, maisha yakuadhibu
Jalali kwako tabibu, Mola Atakujaliya

Umeshakata tama, kifo kwako suluhisho
Imekuwa ja kiama, umefika kweli mwisho
Wahisi ndio nakama, yamekutoka majasho
Mtupie lako jicho, Jalali ‘takujaliya

Huenda ‘medhalilika,huna asili fasili
Pia umebagulika, mejawa nayo fedheli
Umezidi nyanyasika,nao hao mafahali
Kwake wewe ni asali, Jalali ‘takujaliya

Jalali alokuyumba,Anao wako mpango
Yeye Wayuda simba,Atakufuta simango
Jongea zidi kuomba, ‘takufungulia lango
Ahadiye si uongo,Jalali ‘takujaliya.

**Jitathmni**

1.Eleza aina la shairi jipe moyo
2.Lipe shairi jipe moyo kichwa kingine
3.Eleza mbini za kishairi zilivyotumika katika shairi
4.Andika ubeti wa kwanza katika lugha nathari au ya kawaida

## NIFUNZE HEKIMA

**Mtunzi: Kelvin Njoroge**
**Lakabu: Ustadh Muturi**
**Gatuzi: Transnzoia**

Jalali Mtakatifu, nifunze yako hekima
Nijue uadilifu,haki isimame wima
Nepulie udhaifu,kwa kunipa ufahama
Nikiikosa hekima, naishia mpumbavu

Hekima ni kamilifu,pasi hilo ni upuzi
‘tende haki kwa unyofu,amani niwe mjuzi
Jalie utimilifu,hekima ndio azizi
Nikiikosa hekima,naishia mpumbavu

Nielewe ya kutenda, niwe wakutamanika
Ufisadi ukivunda,niwe marashi hakika
Niweze haki kutenda, kwako niweze kufika
Nikiikosa hekima,naishia mpumbavu

Ni duni yangu akili,pasipo hekima yako
Hekima ndio asili,elimu yetu potoko
Ninatenda ya fiili,nifunze mashauri yako
Nikiikosa hekima,naishia mpumbavu

Nabatisha duniani,nisijue kuhukumu
Niondoe ukiwani,hekima nipe Rahimu
Niepulie huzuni,matakwa yako nikimu

Nikiikosa hekima,naishia mpumbavu.

**Jitahtmini**

1..Eleza maudhui ya shairi-Nifunze hekima
2.Nifunze hekima ni shairi la aina gani?
3.Eleza uhuru wa ushairi ulivyotumika
4.Shairi nifunze Hekima lina mishororo mingapi?
5.Mwandishi anaomba nini katika shairi hili?

**NDIMI MTAMBI NATAMBA**
**Mtunzi: John Ngari**
**Lakabu: Malenga wa Mji Mkuu**
**Gatuzi: Embu.**

Ndimi mlumbi nalumba, taa imekosa tambi,
Ndimi ngoi nakuamba, gizani mepiga kambi,
Alosheheni ulumba, kazima vyenu vitimbi,
Ndimi mtambi natamba, ngoi ulo mwana mwambi.

Ndimi yule siyerengwa, siyerengwa kama mbole,
Ndimi yule siyetengwa, siyefanywa golegole,
Yule katu siyeingwa, ili niwe mtefyele,
Kamwe mimi sitotingwa, mevutilia ja kele.

Ndimi sili ulofuvu, nileje uliokuvu,
Ndimi sili ulo’ndavu, vikichelema huwa bovu,
Sipendi ulo’chowevu, kama jani la mnavu,
Ulioliwa na mavu,’kan’achia ukamvu.

Sili usio wagivu, uso na chake kitovu,
Sitala uso mkavu, nika’ndama upotovu,
Siwi katu kitotovu, kujitia kwenye ngavu,
Heri niwe mkulivu, bongo liwe kwenye livu!

Msambe niliyowamba, sambi munayoniamba,
Msambe yalo mafamba, mkaanza kujigamba,

Kunitoa yangu magamba, ili niwe kama ng'amba,
Usiambe kunichamba, ili ukweli kufumba.

Sisemi kwa kujigamba, ili niwe moja namba,
Siachi kutambatamba, hadi nikataratamba,
Aliye wakombakomba, akawafanya miamba,
Ndimi ngoi nakuamba, siambi kwa kujigamba.

Ndimi ngoma muuwamba, ukweli bila kufumba,
Ulo mkwea mikwamba, sifa kuzipambapamba,
Asopenda kuwaamba, bure kuwachambachamba,
Mambo yanukayo vumba, kufanya waja kuvimba.

Tamati nashika kamba, mwisho namaliza ngwamba,
Siambi yalonikumba, kisogo sije niramba,
Sitambi kwa kujigamba, bila ya watu kubemba.

Jitathmini.

1. Taa ya utambi mmoja huitwaje?
2. Taja maneno yaliyoandikwa kwa ufupi
3. Shairi hiki Lina mishororo mingapi jumla?
4. Sheria za utunzi wa mashairi huitwaje?
5. Shairi lisilofuata arudhi huitwaje?

**LIKIZO**
**Mtunzi: Stephen Oluoch**
**Lakabu: Azalisteve**
**Gatuzi: Migori.**

Ajabu hino ajabu,tamu kugeuka chungu
Nilichodhani tabibu,hakileti raha kwangu
Kinanipa masaibu,mambo kutia ukungu
Likizo hauna ladha,sikutaki wachukiza

Kweli umekaa sana,nasihi sasa ondoka
Budi sina kukukukana,za kwako nimeridhika
Huna raha ni khiyana,na zani sizo mipaka
Likizo hauna ladha,sikutaki wachukiza

Sipendi tena nyumbani,shughuli zanitatiza
Natamani vya shuleni,masomo kuendeleza
Nikazame kitabuni,giredi kutengeneza
Likizo hauna ladha,sikutaki wachukiza

Mefanya nimesahau,kitambo niloyasoma
Misemo nazo nahau,siwezi tena kutema
Kazi kukula pilau,nawanda huku nazama
Likizo hauna ladha,huagii wachukiza

**Jitahtmini**:
1.Ni nani mnenaji katika shairi hili
2.Eleza madhari ya shairi hili
3.Kwa nini mshairi anapinga likizo
4.Toa kichwa cha shairi hili

**MAMA YANGU**
**Mtunzi: Stephen Oluoch**
**Lakabu: Azalisteve**
**Gatuzi: Migori.**

Nakupenda mama yangu,hakuna akushindiye
Kukulinda kazi yangu,amani nikupatiye
Nitumia mali yangu,maisha ufurahiye
Mama Jeni mama yangu,pokea heshima zako

Kati ya watu muhimu,nakuweka namba wani
Naomba mungu udumu,unifae maishani
Kwa nyimbo zako matamu,uniondoe huzuni
Mama Jeni mama yangu,pokea heshima zako

Ulicheka nikicheka,beleko kunibebea
Hatarini kunishika,ulinzi hukulegea
Hata katika talaka,mama ulinitetea
Mama Jeni mama yangu,pokea heshima zako

Ulipitia machungu,nashindwa kuhesabia
Ukawa mwalimu wangu,lugha ukanifunzia
Nazungumza kizungu,mwanao nafurahia
Mama Jeni mama yangu,pokea heshima zako

Kalamu naweka chini,hapa natia kikomo
Nikafike kibandani,nifurahishe  mdomo

Chakula nitie ndani,nikarudie masomo
Mama Jeni mama yangu,pokea heshima zako

Jitathmini:

1.Taja aina ya shairi hili
2.Kulingana na mshairi mama ana umuhimu gani katika jamii
3.Taja sifa za mama kulingana na mshairi
4.Mshairi anampangia nini mamake
5.Chambua maudhui ya shairi hili